ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tano – Tarehe 26 Januari, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Ali Mzee Ali) alisoma Dua

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Baraza la Saba la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 15 Oktoba, 2009, Baraza lilipitisha Miswada sita ya Sheria ifuatayo:-

1. Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na Mambo Yanayohusiana na Hayo,

2. Mswada wa Sheria ya Kufuata Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam. 9 ya mwaka 1996 na Kutunga Sheria ya Utalii Zanzibar na Mambo Yanayohusiana na Hayo,

3. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 1996,

4. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya mwaka 1999,

5. Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Yanayohusiana na Hayo na

6. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uzuiaji, Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Nakotiki na Aina ya Sakrotiki na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe, kama inavyotakiwa na kifungu cha 9 91(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2009, naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 85

Wachunga Punda Kuchomana Visu

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Katika mwezi wa Oktoba 2009 lilitokea tukio la vijana wachunga punda kuchomana visu katika maeneo ya Darajani, Mjini Zanzibra. Katika tukio hilo kijana mmoja alifariki.

(a) Je, Mhe. Waziri, vijana waliohusika na kadhia hiyo wamekamatwa.

(b) Kama wamekamatwa, je, wamewahi kupelekwa Mahakamani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba siku ya tarehe 27/10/2009 majira ya saa 6.00 mchana hapo Darajani walitokea vijana walioshambuliana kwa kutumia kisu na panga, ambapo kijana mmoja alikatwa mkono wa kushoto kwenye kiganja na mwengine kisu cha mbuvu na wote walijeruhiwa mkono wa kushoto.

Majeruhi wote wawili walilazwa Hospitali ya Mnazimmoja kwa siku kadhaa na baadaye kuruhusiwa kurejea nyumbani. Katika hao hakuna mtu aliyepoteza maisha katika tukio hilo.

(b) Katika tuko hilo watuhumiwa watatu walikamatwa na kufikishwa Mahakamani na kesi yao bado inaendelea.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa vitendo hivi vya vijana au watu hawa vya kukurupuka tu na kugombana na kuathiri wenzao au kuwapotezea maisha.

Kwa mfano kama tukio hilo lililotokea Darajani na jengine lililotokea Kianga, ambapo alivamiwa msichana kufanyiwa vitendo viovu kwenye *Clubs* za Pombe

na matokeo yake mwisho kupoteza maisha. Kwa kweli hivi sasa vimekuwa vingi sana vinajitokeza katika nchi yetu. Je, wizara yako imejipanga na kujiandaa vipi katika kuyapunguza au kuyaondoa kabisa masuala haya?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Jeshi la Polisi tunajitahidi sana kutoa taaluma kwa wananchi wetu na zaidi hivi sasa tunao utaratibu wa kuanzisha Polisi Jamii, kwa ajili ya kuweza kupata taarifa za wahalifu mbali mbali na kuweza kuwafanyia kazi.

Pamoja na hayo matukio machache yaliyotokezea, lakini kutokana na jitihada za Jeshi la Polisi. Kwa kweli matukio mengi tumeweza kuyadhibiti na kama sio utaratibu ambao tunautumia kwa kushirikiana na wananchi, basi jamii yetu ingekuwa katika mtafaruku mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba sana wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi na zaidi kushirikiana na Masheha katika kuanzisha Ulinzi Shirikishi Jamii kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, kwa ajili ya kuweka amani, usalama pamoja na utulivu kwenye maeneo yetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali mmoja la nyongeza. Mhe. Waziri, katika kipindi hiki Zanzibar matukio ya uhalifu, kuporwa watu simu zao, kukabwa watu, kuchomwa visu ni masuala ambayo yamekithiri sana.

Vile vile, inafahamika kwamba kila kwenye maeneo kuna watu maalum ambao wanafanya vitendo hivyo na wanajulikana, lakini wanapofikishwa mikononi mwa Jeshi la Polisi, basi watu hao baada ya siku ya kwanza au ya pili huachiliwa.

Je, haoni Mhe. Waziri kwamba watu hawa wakikamatwa na kupelekwa polisi na baadaye kuachiliwa, inasababishwa na wengine kuona kuwa hakuna matatizo yoyote na kuendelea kufanya kama hivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inafuata Utawala Bora na kama ingelikuwa enzi zile za zamani, basi kama unamuona mtu ameiba simu na ukimpeleka na kusema kwamba huyu nimemuona ameiba simu, basi anaambiwa ahesabu ngazi. Lakini hivi sasa nchi yetu inafuata Utawala Bora, inabidi lazima upatikane ushahidi wa kutosha na hata kama wewe mwenyewe unaona lile tukio lenyewe, lazima upatikane uthibitisho. Kwa hivyo, tatizo linalojitokeza Mhe. Mwenyekiti, kwamba watu wetu hawataki kuwa mashahidi na hilo ndilo tatizo.

Sasa Mahakama bila ya kuwa na ushahidi hawawezi kumtia mtu hatiani. Kwa maana hiyo, tatizo la wananchi wetu wakati mwengine linatokezea tukio kama alivyosema Mhe. Mjumbe, kwamba wapo watu wezi maarufu na wanajulikana mitaani, lakini nani mwenye kwenda Mahakamani kwa ajili ya kuwa shahidi kwamba fulani ndiye aliyefanya jambo fulani, kwa kweli hili ndilo tatizo letu.

Mhe. Mwenyekiti, ndipo pale niliposema kuwa tunawaomba sana wananchi wetu kushirikiana na Masheha kupitia katika Ulinzi Shirikishi Jamii, ambapo Jeshi la Polisi wenyewe ndio wanaoongoza zoezi hilo, kwa ajili ya kuweza kusaidia usalama katika maeneo yetu.

Kwa kweli wananchi wetu wanaogopa lawama, kwa sababu wezi tunawajua ikiwa tunakaanao mtaani, bila ya shaka itakuwa ni majirani zetu. Lakini mtu anaogopa kuwa shahidi kwa sababu fulani ataniona mbaya kwa kuwa nimekuwa shahidi kwa mwanawe kutiwa hatiani.

Kwa hivyo, narejea tena Mhe. Mwenyekiti, kwamba ulinzi ni wetu sisi wenyewe kwa usalama wetu pamoja na mali zetu, basi tukiweza kutoa ushahidi hata Jeshi la Polisi tutaweza kuwasaidia katika kazi hii ya kuwakamata wahalifu na kuwafikisha Mahakamani na sheria kuchukua mkondo wake.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri katika majibu yake mazuri ametoa wito kwa wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha kwamba amani inapatikana.

Lakini hivi karibuni kumekuwa na shutma nyingi kuhusiana na Jeshi la Polisi kuhusikana na matukio mbali mbali ya kihalifu, yakiwemo ya mauaji na ujambazi. Je, anatoa wito gani ili tuweze kujenga imani nao.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, suala la shutma kwa Jeshi la Polisi kujihusisha na kitendo vya ujambazi au mauaji. Kwa kweli mimi bado sijazipata. Isipokuwa kimsingi suala la ujambazi na uhalifu ni suala ambalo halina kinga kwa Jeshi la Polisi au askari mwengine yeyote. Kwa sababu mtu yeyote anapofanya vitendo vya ujambazi, basi hata kama askari ina maana vile vyeo vyake anavivua na kuwa jambazi, ikiwa anajihusisha na masuala ya uhalifu basi haisabiki kama ni polisi, kwa sababu lile tukio amelifanya yeye mwenyewe bila ya kutumwa na mtu.

Kutokana na hali hiyo, kitu tunachokiomba ni kwamba tuhuma ya askari yeyote anayetuhumiwa katika matukio kama haya, basi tunaomba Waheshimiwa Wawakilishi, viongozi wengine mbali mbali pamoja na wananchi kwa jumla, kuweza kutupa taarifa na kuwafanyiakazi na ikiwezekana tukipata uthibitisho

kuweza kuchukua hatua za haraka. Lengo ni kuendelea kulinda heshima ya Jeshi la Polisi hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Nam. 50

Kukatika kwa Umeme Mara kwa Mara

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Pamoja na jitihada za dhati za serikali za kuwapatia wananchi wake huduma ya umeme, bado suala la kukatika kwa umeme Unguja na Pemba limekuwa ni donda ndugu. Hivi karibuni tumeshuhudia umeme kukatika tena baada ya kuharibika kwa mitambo ya kupokelea umeme huko Fumba.

(a) Ni sababu zipi zilizochangia kuharibika kwa mitambo hiyo.

(b) Mbali na hasara kubwa waliyopata wananchi kimaisha na kiuchumi, serikali ilipata hasara kwa kiasi gani.

(c) Kutokana na hali hiyo ambayo si mara moja kutokea, je serikali bado haijaona haja ya kutafuta chanzo kingine cha umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, sababu kubwa iliyochangia kuharibika kwa mitambo hiyo ni uchakavu wa mitambo yenyewe, ambayo hivi sasa imeshafikia umri wake iliyokadiria.

(b) Kwa upande wa Shirika la Umeme mbali na hasara za matengenezo ya mfumo wa umeme huko Fumba, pia limepata hasara ya makusanyo na mauzo ya umeme hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2009, jumla ya shilingi bilioni mbili zimekosekana.

(b) Ipo haja ya kutafuta chanzo mbadala cha kuzalisha umeme, ndio maana serikali imo mbioni katika jitihada zake za kuhakikisha kuwa vinanunuliwa vinu vya kuzalisha umeme vya angalau megawati 25.

Vile vile, haja hiyo imesisitizwa sana jana,na karibu wote waliopata fursa ya kuchangia Sera ya Nishati Zanzibar, wala hakuna ambaye amezungumza ikawa hakuzungumza juu ya suala la kuwa na umeme mbadala.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa umeme hivi sasa Unguja haupo zaidi ya mwezi na wananchi hawapati taarifa za mara kwa mara kwa hatua zinazoendelea, baadhi ya wananchi hudai kuwa hakuna hatua zinazochukuliwa. Je, Mhe. Waziri anaweza kuaambia wananchi hatua iliyofikia, ili kuondoa ile dhana ya kwamba hakuna kinachoendelea? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa zaidi ya mwezi hivi sasa hapa Unguja imekosekana huduma ya umeme na mara chache tumekuwa tukitoa taarifa ya hali inavyoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Baraza lako tukufu napenda niwajuilishe na kuwahakikishia Wajumbe wako wa Baraza na wananchi kwa jumla, kwamba kazi za matengenezo ya *cable* zinaendelea na kama Mhe. Waziri alivyotoa taarifa na kutaja zile tarehe ambazo matumaini yetu ya umeme yatarejea iko pale pale.

Vile vile, hata juzi Mhe. Waziri alinitaja mimi mwenyewe binafsi niende kule Ras Kilomoni, ambapo leo asubuhi nilikuwa nikiwasiliana na Meneja wa Shirika la Umeme na tumekubaliana kimsingi siku ya Jumatatu au Jumanne nitakwenda kule Ras Kilomoni.

Kwa hivyo, nataka niwathibitishie wananchi kwamba mafundi tayari wameshafika na kazi za ukarabati wa umeme huo zinaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongezea kidogo juu ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri kuhusu mwenendo mzima wa kurejesha umeme Kisiwani Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, tumetoa taarifa na tulisema tatizo kubwa ambalo lilikuja kuturejesha nyuma na kutupotezea muda ni kupoteza kwa wiki tatu hadi nne za kipindi cha mwisho wa mwaka kutokana na Sikukuu za *Christmas* na mwaka mpya, ambapo kwa kipindi cha wiki nne wenzetu Ulaya hawafanyikazi.

Kwa mnasaba huu wa vifaa vingi tulikuwa tunavitegemea kutoka Sweden kwenye Kampuni ya *ERICSON* nyote mnaifahamu, kwa kweli hii ni kampuni

ya kimataifa yenye sifa kubwa. Tuliamua kwa makusudi kufanya hivyo kutokana na hali halisi ya maamuzi yetu sasa kugeuza mfumo mzima wa vituo vyetu vya Ras Kilomoni na Ras Fumba.

Ninafuraha ya kutoa taarifa kwamba hivi sasa zaidi ya asilimia 90 ya vifaa vyote ambavyo tunahitaji kuanza urejeshaji wa umeme vimeshafika. Mhe. Mwenyekiti, jana kuna shehena moja imetoka Nairobi na tunategemea nyengine leo itatoka Nairobi, waya tunaouhitaji umeshafika na makombe ya kuunganisha waya huo yameshafika.

Isipokuwa hivi sasa tunachokisubiri ni mafuta ambayo yanatumika kupoozea waya wenyewe na tunategemea kupata mapipa kumi na mbili kutoka Uingereza, ambayo yanachukuliwa leo na Kampuni ya *DHL* na kuanza utaratibu wa kuletwa Unguja, baada ya hapo vitabaki viungio viwili tu ambavyo tunategemea kuvisubiri kutoka Sweden. Lakini siku ya Alhamisi kwa taarifa niliyopewa na mafundi jana wananza kazi ya kuunga taratibu hivi sasa.

Pamoja na hayo, tumetoa taarifa kwamba shughuli hiyo tunategemea kuikamilisha tarehe 20 Februari, 2010. Lakini bado matumaini yetu ni kwamba kufanyakazi ili urejee kabla ya tarehe 20.

Pia, tunategemea wiki hii watakuja wataalamu kutoka Kampuni ya *NEXANS*, ambayo ilitengeneza waya wenyewe. Mtaalamu mmoja wa mkonge wenyewe kwa maana ya waya wenyewe kuja kuukagua kwa ndani kabisa, yaani kufanya ukaguzi wa kina wa waya na mwengine ni mtaalamu wa mafuta ya kupozea waya wenyewe. Kwa hivyo, tunategemea kwa ile ratiba tuliyoitolea taarifa tunaendelea nayo vizuri.

Isipokuwa naomba nidokeze kidogo pamoja na taarifa nyengine ya faraja, ambayo tayari tulikuwa tumeshaitolea taarifa hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Baraza hili lilisisitiza sana na hata alivyozungumza Mhe. Naibu Waziri kwamba wakati tulipokuwa tukichangia Sera ya Nishati Zanzibar kuhusu umeme wa akiba, kwa maana hatuazimi ni wetu wenyewe wa kuzalisha kwa vinu.

Kwa hivyo, tunaendelea na jitihada ya kujenga misingi hiyo Unguja na Pemba, kwa maana vile vya Pemba vilivyopo tuviendeleze na tuongezee na Unguja tuvitafute. Kutokana na historia yetu ya miaka mingi sana vinu vya akiba vimepotea.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa maana ya Baraza la Mapinduzi limeiagiza wizara yangu kuingia katika harakati za manunuzi ya majenereta. Serikali

imeagiza kwamba tushirikiane na Serikali ya Norway, ambayo ndio kiongozi katika Washiriki wa Maendeleo kwenye Sekta ya Nishati hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Serikali ya Norway tulipowaomba tu, basi waliwapa kazi *Norplan* ni kampuni ambayo iliyosimamia usambazaji umeme vijijini tokea hatua ya mwanzo mpaka mradi huu wa Pemba. Kwa kweli ni kampuni ambayo inaaminiwa sana na Serikali ya Norway pamoja na sisi wenyewe.

Kutokana na hali hiyo, wale wakaingia kwenye harakati za kututafutia watu wa aina mbili. Moja ni hawa *Independent Power Producers*, yaani wanaozalisha umeme kama vile *DOWANS* na wengine. Kwa hivyo, wamealikwa wale na kuleta tathmini ya kuweza kuleta vinu kwa ajili ya kuzalisha umeme, wengine wametafutwa na watakuwa tayari aidha kutukodisha au kutuuzia vinu vya kuzalisha umeme moja kwa moja.

Kwa kweli tumekwenda na harakati hizo karibu ya wiki tatu hivi sasa na makampuni mengi yamejitokeza kwa nyanja zote mbili hizo nilizozizungumza na hatimaye hivi sasa tuko kwenye taratibu za kuandaa mikataba ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba zaidi ya Dola Milioni kumi na mbili tulizozihitaji, yapo matumaini makubwa kuwa zote hivi sasa tumeshazipata. Hivyo, tumo kwenye harakati za kuandaa mikataba ya mwisho, pia tumo kwenye harakati za kutizama njia nyepesi za kusafirisha vinu hivyo kuja hapa Unguja. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunayo matumaini makubwa kwa wale waliotuahidi kutupa fedha zao na kwa wakati, serikali kwa upande wake imejiandaa na hii leo kampuni hiyo imeleta mafundi wake, kwa ajili ya kuanza michoro ya *foundation* ya kuweka *generators* hizo kule Mtoni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametufungulia njia nyengine kutokana na shida hii tuliyoipa na kwa uwezo wake tutaweza kukamilisha kazi hii kwa haraka na waya wetu utakubali kutengenea safari hii. Vile vile, harakati hizi za kuleta *generators* zitakamilika kama tulivyopanga. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Nishati Mbadala napenda kudokeza kidogo taarifa, kwamba kule Pemba katika harakati zetu za kuwashajihisha watu kutumia jua, upepo na kadhalika, ili tuanze kupata nishati hiyo sasa. Kwa mfano kuna mradi mmoja mdogo ambao tumejaribu na tayari umeshaunganisha na *grid* ya Pemba wa *kilovolt* 12 elfu. Taasisi moja ambayo ni *Non-Government Organization* yenye Makao Makuu yake Ujerumani, katika zoezi la mwanzo hilo ambalo limeanza kwa muda sasa.

Lakini tunategemea baada ya kikao cha Baraza mimi na wenzangu tutautembelea mradi ule, kwa ajili ya kuendelea kuingia kwenye mazungumzo na hawa watu kutizama na kuweza kupanua wigo ule na kuingia nao mikataba ya kibiashara ikiwa tutaweza kuridhiana. Kwa hivyo, tunaendelea na upande huo pia, ili kujiwekea usalama zaidi katika upatikanaji wa nishati katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ahsante sana kwa maelezo yako na hii ndio kazi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kwenye mpira kuna watu ambao wanaotizama, basi kunakuwa na watu anaokwenda huku na kule na wala hawachezi wao.Kwa hivyo, na mimi niko huku kwenye kiti, sasa wakati mwengine munistahamilie. *(Kicheko/Makofi)*

Ninawambia Mhe. Spika, siku hiyo kama atanipanga hapa basi nitaweka kanuni pembeni na nitachangia, lakini *Inshaallah* haitofika hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Nam. 67

Matatizo Yanayoikabili Sekta Binafsi

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Sekta Binafsi ni muhimili wa uchumi wetu na ndio inayochukuwa watu wengi katika ajira. Lakini bado inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo mazingira mabaya ya kibiashara, utitiri wa kodi na wingi wa vyombo vinavyokusanya kodi hizo.

(a) Je, wizara imeandaa mikakati gani kukabiliana na matatizo hayo ili kutoa nafuu kwa sekta hii.

(b) Je, mabenki yetu yanaisaidiaje sekta hii kukua.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba nikupongeze kwa furaha uliyonayo leo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ahsante nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kukabiliana na mazingira mabaya ya kibiashara, utitiri wa kodi na wingi wa vyombo vinavyokusanya kodi, Wizara ya Utalii, Biashara ya Uwekezaji kwa kushirikiana na wizara nyengine za serikali imeandaa mikakati mitatu ifuatayo:-

- Kufanya mapitio ya Sheria tatu (3) zinazosimamia uendeshaji biashara kupitia Mpango wa Kuimarisha Mazingira Bora ya Biashara Tanzania (*BEST*), ambazo ni Sheria Nam. 2 ya mwaka 1995 ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji. Sheria Nam. 4 ya mwaka 1983 ya Mizani na Vipimo na Sheria ya Biashara Nam. 4 ya mwaka 1989.

- Kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Utawala Bora, yaani Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, wizara inafanya mapitio na mfumo uliopo wa utoaji leseni za biashara na kuweka upya, ambao unaleta ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa leseni na kupunguza gharama za upatikanaji leseni hiyo (*One Stop Centre*).

- Kwa kupitia mikutano ya Baraza la Biashara (ZBC), Kamati ya Pamoja ya Mageuzi ya Mfumo wa Kodi, iliagizwa kuangalia malalamiko mbali mbali ya Sekta Binafsi juu ya kuweko kwa utitiri wa kodi na baadaye kuwasilisha mapendekezo yake serikalini, na kazi hiyo imekamilika na sasa inafanyiwa kazi na Wizara ya Fedha inayosimamia shughuli hiyo.

b) Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mabenki kwa kweli mabenki yamekuwa yakitoa mikopo kwa wafanyabiashara ingawa

wafanyabiashara wadogo wadogo walishindwa kutumia mikopo hiyo kwa sababu kadhaa, moja ikiwemo ukubwa wa riba katika mikopo hiyo lakini pia na masharti mazito ya mikopo. Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hatua kadhaa zinachukuliwa kwa upande wa sekta ya fedha kupitia mabenki yakuweka vitengo vitakavyosaidia wafanyabiashara wadogo wadogo. Moja kati ya mipango hiyo ni kuanzisha vitengo vya *Islamic Bank* ambayo maadili yake hayana riba. Mpango huu umo ndani ya *Bank* ya *FBME* lakini pia Benki ya Watu wa Zanzibar nayo imeshaanzisha. Kwa hivyo, ni matumaini yetu kwamba na mabenki mengine yatafuata.

Mhe. Mwenyekiti, benki nyengine ambayo inatoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ni *NMB* ambayo hivi karibuni wameshafungua tawi lao hapa Zanzibar na nimatumaini yetu kwamba wataanzisha huduma hizi kwa haraka.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu hayo mazuri kutoka kwa Mhe. Waziri, napenda niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wafanyabiashara ndogo ndogo wengi ni wanawake na kwa kuwa wanawake wana mitaji midogo ya kibiashara na kwa vile pengine hawazifahamu taratibu za kukopa benki.

Je, wizara yake ina mpango gani wa kuwasaidia wajasiriamali hasa wanawake, nao pia wakaweza kupata mikopo kwa ajili ya kuendesha biashara zao na wakajua mbinu gani wafanye ili waweze kuitumia vizuri hiyo mikopo ya benki na baadae waweze kurejesha ili waweze kwenda mbele na biashara zao?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima wanaendesha mafunzo ya aina mbili. Mafunzo haya kwa jina moja tunaita Jitegemee Kibiashara na katika mafunzo haya kuna aina tatu za mafunzo na yote yanafundisha jinsi ya kufaidika na mikopo mbali mbali inayotolewa sio tu na benki, lakini hata taasisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya mafunzo haya pia kuna mitaji midogo midogo inayosaidia wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuendesha biashara zao. Kwa hivyo, nitoe wito tu kwa wafanyabiashara wote na nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza wanawake katika mpango huu wanawake wamejitokeza wengi ukilinganisha na vijana wanaume. Kwa hivyo, nitoe wito tu kwa wote vijana na wanawake kujitokeza kwa wingi katika mpango huu ulioandaliwa na Sekta Binafsi ya Tanzania ili wafaidike na mitaji inayotoka katika mafunzo ya aina hiyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri amekiri katika jawabu mama kwamba kuna utitiri mkubwa wa kodi na hivi sasa wamo mbioni kurekebisha baadhi ya sheria.

a) Katika utitiri huo wanaohusika sana ni Manispaa na Halmashauri za Wilaya. Je, wameshirikishwa katika zoezi hilo.

b) Hivi sasa katika nchi yetu kumezuka mabenki mengi kuja kuekeza, lakini wananchi pamoja na wafanyabiashara wakikopa riba zinakuwa kubwa badala ya kupungua. Je, hii inasababishwa na nini?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, katika kulifanyia kazi suala la utitiri wa kodi Manispaa wameshirikishwa na Halmashauri za Wilaya pia wameshirikishwa. Suala la riba kwa mabenki naomba niseme kwamba mabenki ni wafanyabiashara na mfanyabiashara kazi yake ni kuongeza faida kwa upande wake. Lakini kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba mabenki haya sasa hivi yanafungua vitengo maalum ambavyo havitakuwa na riba. Kwa hivyo, niwaombe tu wananchi kufuatilia mipango hiyo na kuelekea huko katika kukopa kwao.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri, hii mikakati ambayo kwamba imeandaliwa itachukua muda gani.

b) Bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar haina matatizo yoyote, lakini bidhaa kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara zina matatizo makubwa sana. Je, wizara yake imechukua hatua gani kurekebisha hatua hizo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, mikakati iliyopangwa haitachukua muda mrefu kwa sababu baadhi ya sheria zitawasilishwa katika Baraza lijalo la mwezi wa April ili kwa pamoja tuzifanyie marekebisho zianze kutumika.

Lakini suala la pili la bidhaa kwenda Bara suala hili ni la muda mrefu na tumelifanyia kazi sana kupitia wizara pamoja na kamati yetu maarufu ya kero za Muungano. Kwa hivyo, tumelifanyia kazi kwa muda mrefu sana na baadhi ya matatizo yameanza kuachia achia sasa hivi ingawa bado kuna ugumu fulani, lakini mengi ya yale matatizo yameanza kulegea na malalamiko yamepungua.

Nam. 19

Mtaro na Barabara ya Uwanja wa Ndege

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Uchimbaji wa Mtaro wa maji ya mvua na matengenezo ya barabara ya uwanja wa ndege Zanzibar umewezesha kuondoa tatizo la maji kutuwama katika barabara hiyo, lakini mtaro huo haukujengwa baada ya kuchimbwa.

(a) Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja kwa mtaro huo kufanyiwa ujenzi wa kudumu ili kuuimarisha.

(b) Kazi iliyofanyika ya uchimbaji wa mtaro na ujenzi wa barabara hiyo umegharimu serikali kiasi gani cha fedha mpaka ilipofika.

Mhe. Naibu wa Mawasiliano na Uchukuzi- Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 kama ifuatavyo;-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa mtaro wa maji ya mvua uliojengwa katika barabara ya Uwanja wa Ndege Zanzibar umewezesha kuondoa tatizo la maji barabarani, na ni kweli kuwa mtaro huo bado haujakamilika. Wizara haijakamilisha mtaro huo kutokana na kujitokeza kwa kuingia maji ndani ya majumba ya wananchi wa jirani na mtaro huo. Tunalitafutia ufumbuzi tatizo hilo na mara tu baada ya kusawazisha kasoro hiyo basi mtaro huo utakamilika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mpango huu wa mradi wa mtaro wa maji ya mvua maeneo ya Uwanja wa Ndege umesaidia sana kuondoa kero ambayo barabara ile sasa hivi inapitika bila ya matatizo. Lakini kwa bahati mbaya kuna wananchi ambao katika kupita mtaro ule, kulikuwa kuna daraja ambazo wanapitishia gari na mambo mengine wamezuilika hadi leo hazijarudishwa daraja zile, ili kurudishwa wanaambiwa kwamba walipe shilingi laki moja kila mtu.

Je, hii ni kweli na kama kweli kwa nini ifanyike hivyo wakati Idara ya Barabara ni muhusika mkuu wa shughuli yote iliyofanyika katika eneo hilo?

Mhe. Naibu wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika maeneo ambayo barabara inafanyiwa matengenezo kunakuwa na matatizo mbali mbali yanajitokeza ikiwemo hizo sehemu ambazo za kupitisha magari, lakini hilo ni jukumu la wizara yangu. Kwa hivyo, namuhakikishia kwamba maeneo yote ambayo hayajajengwa basi tutayafanyia kazi.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa swali mama lina (a) na (b) na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amejibu (a) na (b) ameiacha tujaalie kuwa hili (b) halina jawabu.

b) Lakini kulingana na michoro iliyopo na mtaro ule, mtaro ule unatarajiwa kuwa wa aina gani wa kufunika juu au wa kuwa wazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, hadi sasa mtaro ule umeshagharimu karibu shilingi milioni mia mbili na thalathini. Pia, tunatarajia utakapomalizika tutafunika juu ili wananchi wasiweze kupata madhara.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba pamoja na Mhe. Naibu Waziri kujibu kwamba ni wajibu sisi wizara kurejesha vile vikuta alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali, lakini tayari sehemu nyengine kama pale kwa Kira ipo sehemu ambayo gari zinapita na kuingia ndani. Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni jukumu letu kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kazi iliyofanywa aliyoeleza Mhe. Waziri kulichimbwa shimo kubwa sana hii barabara inayokwenda *Airport* ya zamani na shimo lile hadi leo lipo na lilikusudiwa kwamba maji yanayotoka kule yaingie pale.

a) Je, Mhe. Waziri anaweza kulieleza Baraza hili kwamba shimo lile lilichimbwa kwa kubahatisha tu au ulikuwa ni uamuzi mahsusi wa serikali.

b) Shimo lile liligharimu kiasi gani.

c) Haoni kwamba maji yanayotuama pale yatasababisha mazalio ya mbu na yataleta malaria jambo ambalo serikali inapiga vita.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, mchakato wa ujenzi wa mtaro ule ulianza muda mrefu kidogo kwa hatua mbali mbali na matarajio mengi. Katika hatua za kwanza ndio pamoja na kuchimba hilo shimo kwa matarajio kwamba tutafanikiwa kuondoa maji. Lakini hatimae ilionekana kwamba maji ambayo yanatoka milimani kuwa eneo la Kiembesamaki ni mengi na yanatoka sehemu nyingi. Kwa hivyo, baada ya wataalamu wetu kukaa kwa mara ya pili na kuangalia tufanye nini ndio maana wakaja na wazo hili la awamu ya pili. Gharama za shimo lile na hizi nyengine zote ndio hizo ambazo nimezitaja awamu ya kwanza na awamu ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali ni kuona kwamba wananchi wote wa Kiembesamaki hawadhuriki, lakini barabara ile ni muhimu kwa nchi yetu kwa hivyo ndio maana juhudi kubwa za serikali zimewekezwa pale katika kumaliza tatizo la kutuama maji barabarani na kwenye nyumba za watu wa Kiembesamaki.

Nam. 111

Marufuku kwa Matangazo ya Pombe na Mchezo wa Ngumi Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Abass Juma Muhunzi) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu katika michezo umekuwa ni utamaduni wa timu za Zanzibar kutoshiriki katika mashindano ambayo yanatangaza pombe pamoja na kutoendesha mashindano ya mchezo wa ngumi (Masumbwi).

(a) Je, Mhe. Waziri, ni kwa nini utamaduni huu mara hii umevunjwa pale Timu ya Mpira wa Miguu ya Mafunzo iliposhiriki katika Mashindano ya Kombe la *Tusker* ya Tanzania Bara.

(b) Wizara yako imefanya utafiti ili kugundua kuna udhaifu gani katika Timu ya Mafunzo uliopelekea kapata kipigo kikubwa cha kufungwa mabao 6-0 kwa Timu ya Yanga ya Dar-es-Salaam ambayo si timu ngeni kwa Mafunzo.

(c) Kwa kuwa vijana wetu sasa wanashiriki katika mashindano ya Judo na Ngumi za mateke (*Kick Boxing*) ambayo haina tafauti sana na mchezo wa Ngumi wa kawaida (*boxing*). Je, hii ni kusema sasa mchezo wa ngumi nao unaruhusiwa kuendeshwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti,kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 111 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, swali hili nimejitahidi sana kujibu kwa kina wakati tukitoa ufafanuzi juu ya Mswada wa Sheria Nam. 7 ya Tume ya Utangazaji hapa Zanzibar ambayo ilieleza kwa undani kabisa.

(a) Mhe. Mwenyekiti, si utamaduni wetu kwa timu za Zanzibar kutangaza ama kushiriki katika mashindano ambayo yanatangaza pombe kwa hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, utamaduni wetu hauruhusu matangazo ya pombe na sigara kwenye viwanja vyetu vya mpira, michezo yetu mbali mbali ya kila aina ndani ya mipaka ya Zanzibar kama ilivyokuwa nchi mbali mbali katika sera zake ikiwemo nchi ya Ufaransa pamoja na nchi nyengine nyingi za Mashariki ya Kati ikiwemo Saudia Arabia, United Arab, Oman, Qatar, Bahrain, Malaysia, Kuwait na Mali. Hayo tulifanyia utafiti na kujua pia na wao wanakataza matangazo ya pombe na sigara hususan Ufaransa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haijafanya utafiti halisi kugundua udhaifu uliopelekea timu ya mafunzo kufungwa mabao (magoli) 6 na Timu ya Yanga ya Dar es Salaam. Lakini hali iliyojitokeza siku ya mchezo ilionesha kuwa timu ya mafunzo haikujiandaa vizuri na mashindano hayo ikilinganishwa na wapinzani wao wa Timu ya Yanga ambao walijiandaa vizuri na mashindano hayo na kiwango chao cha uchezaji kilikuwa cha hali ya juu hata kuliko Simba na wao walifanikiwa kuchukua kombe la *Tusker*. Isitoshe timu ya mafunzo ilikuwepo mapumzikoni wakati huo na nje ya kambi ya *league* kuu ya Zanzibar wakati Yanga ilikuwa mashindanoni tayari.

Mhe. Mwenyekiti, Yanga ilijitayarisha vizuri sana na mafunzo yake pamoja na mazoezi na haikuwa mapumzikoni na sababu nyengine anazifahamu Mhe. Mwakilishi, ni mazungumzo ambayo yanafanyika mitaani na sehemu mbali mbali ya hapa Zanzibar ambayo yanaunga mkono sera yetu hiyo ya kuzuia pombe na sigara ndani ya michezo.

(c) Mhe. Mwenyekiti, ninaomba kumjuulisha Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kuwa mchezo wa ngumi za mateke yaani (*kick boxing*) haujaruhusiwa kuchezwa hapa nchini nakuwa ipo tofauti kubwa kati ya mchezo wa Judo na mchezo wa ngumi. Mhe. Mwenyekiti, tofuati ni kuwa katika mchezo wa judo wachezaji hawapigani ngumi wala

mateke isipokuwa wanaoneshana nguvu na mbinu katika kukamatana na kuangushana kwenye kiwanja kilichowekwa matandiko maalum ya kuangukia.

Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wanashiriki mchezo huo wa *kick boxing* na kupata ushindi mbali mbali, lakini ni nje ya mipaka ya Zanzibar. Kama vile matangazo yanayofanyika ya pombe na sigara nje ya Zanzibar na timu zetu kushiriki katika michezo hiyo na viwanja hivyo. Kutokana na michezo hiyo kutotambulika rasmi hapa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, tumeshindwa sisi kuwazawadia ama kuwapokea au kuwasindikiza rasmi pale ambapo wanapokwenda kwenye mashindano ya kimataifa ama kutuletea medali wao wakiwa kama Wazanzibari.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yametutanabahisha kwamba kila timu ijenge mkakati wa kufanya maandalizi mazuri ili iweze kushinda. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kabla sijauliza swali la nyongeza ningemuomba Mhe. Naibu Waziri ile kauli yake aliyosema kwamba katika mashindano ya *Tusker* Timu ya Simba haikujiandaa, lakini nataka nimdhihirishie kwamba Simba ni timu bora katika Tanzania na Afrika kwa sasa hivi kwa sababu imecheza michezo 13 haijapoteza hata mmoja na inaongoza *league* katika historia ya Tanzania na Afrika ubingwa wameshachukua bila ya jasho.

Mhe. Mwenyekiti, maandalizi ni jambo muhimu sana na tukizingatia kwamba timu zetu za Zanzibar ni masikini sana na wafadhili wako wa aina nyingi, lakini kwa kuwa serikali kwa upande wake inasema kwamba timu kupatiwa wafadhili ambao wanatumia nyenzo za pombe haitakiwi, mimi naunga mkono hilo wala sina matatizo.

Kwa kuwa *league* ya mwaka jana ilidhaminiwa na wenzetu wa *ZANTEL* walitumia shilingi milioni 120 kudhamini vilabu vyetu vikapata nguvu vikaendelea na *league* yao bila ya matatizo. Lakini safari hii kwa bahati mbaya kuna tetezi kwamba *ZANTEL* wamejitoa kutokana na *ZFA* wanataka milioni 300

Je, suala hili ni kweli na kama ni kweli wizara kwa kuwa *ZANTEL* wamejitoa imechukua hatua gani za kuhakikisha kwamba wanazungumza na *ZANTEL* ili angalau kurudisha tena ufadhili wao japo kwa zile thamani ya fedha za mwaka jana ili vilabu vyetu tuvisaidie viendeleze *league* yao bila ya matatizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikusema kwamba Simba ilikuwa haijajiandaa, nilichosema mimi Yanga ilikuwa imejiandaa vizuri zaidi kuliko Simba na sikusema kwamba Simba hawaongozi *league* kuu hivi sasa, lakini nilichosema kwamba katika ule mchezo wenyewe unaochezwa wa Yanga unajuulikana.

Mhe. Mwenyekiti, nikijibu swali lake la (b) ni kweli mwaka jana *league* ya hapa Zanzibar ilidhaminiwa na *ZANTEL* na walidhamini kwa milioni 120 na matatizo mbali mbali yaliyotokezea sote tuliyaona kupitia timu na vilabu ambavyo vilileta mizozo juu ya mkataba ule na kutaka kujua undani halisi na vikao mbali mbali vilivyofanyika pale Bwawani na kama kampuni ya biashara ilivyo huwa haipendelei kuingia matangazo yake kwenye mizozo mara nyingi kwa sababu lile linakuwa haliwajengi kibiashara bali linawabomoa. Kwa hivyo, *ZANTEL* baada ya kuona hali hiyo kwanza walitaka kujitoa hapo awali.

Lakini la pili walipopelekewa bajeti kubwa ni kweli wamepelekewa bajeti ya milioni 300 na walipoona bajeti hiyo wakasema hilo watashindwa. Lakini *ZFA* ni chama cha mpira ambacho kimesajiliwa na kina uhuru wake kamili wa kufanya kazi yake. Mpaka hivi sasa sisi kama wizara hatuwezi kuwaingilia ikiwa wao hawajatufuata kutwambia rasmi kwamba jamani tumeshindwa na hilo bado hawajalikubali kwamba tumeshindwa kupata mdhamini wakitamka hilo kama wameshindwa sisi kama wizara na naamini Mhe. Waziri mwenyewe yupo ambaye ni Naibu Waziri Kiongozi hilo kwake ni mara moja kuliingilia na kuweza kupata udhamini, lakini bado wao hawajakubali kwamba wameshindwa na udhamini huo.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kupata fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu jibu mama alisema kwamba Timu ya Mafunzo pamoja na kipigo kile walichopata ilikuwa ni timu nzuri, lakini ndio ilitokezea tu kwa sababu ya matayarisho ya hao Yanga.

a) Haoni kwamba hiyo ilikuwa ni adhabu ya kukiuka kwao maadili na kama hivyo ndivyo ni hatua gani wamechukuliwa ili isije ikatokezea na timu nyengine kufanya hivyo, kwa sababu wakiona wenzao wamekwenda hawakuambiwa chochote na wengine nao watakwenda.

b) Mhe. Mwenyekiti, tulisikia kwamba Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alizuia huu mchezo wa ngumi kwa sababu anasema yeye haoni sababu watu kupigana bila ya kuwa na sababu ya kupigania. Sijui kama hili ni kweli na kama sio kweli Mhe. Naibu Waziri aje kutwambia na hili suala la *kick boxing* ambalo lipo na linasemekana kwamba halijawa rasmi lakini bado lipo. Je, huu ukimya haionekani

kama itakuwa inatoa fursa na mwanya kwamba hii shughuli iendelee na kwa kufanya hivyo itakuwa tunakiuka yale maagizo ya mzee wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa Zanzibar inaongozwa na sheria ambayo hupitishwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na sera mbali mbali ambazo huridhiwa ndani ya Baraza la Wawakilishi na Zanzibar inaongoza miongoni mwa Utawala Bora kwa kuongoza. Kwa hivyo, nikubaliane kwamba Timu ya Mafunzo imepata kipigo hicho kutokana na maadili ambayo wao wenyewe wamevunja, lakini maadili yale hayakuvunjwa ndani ya mipaka ya Zanzibar bali yamevunjwa nje ya mipaka ya Zanzibar. Kisheria sisi hatuwezi kuikataza timu wala klabu kwenda kwenye mashindano yoyote ambayo wanaalikwa nje kwa sababu mashindano yale hudhaminiwa na wadhamini mbali mbali na hata nchi za nje wengine huwa wanapata udhamini wa pombe pamoja na sigara, lakini kwa klabu zetu sisi hatuwezi kuwakataza. Lakini ninachotaka kusema kuna usemi ule wa zamani kwamba “fimbo ya Mwenyezi Mungu huwa haina sauti”.

Kwa hivyo, hata hao wengine wakenda Mundu na nani huenda nao wakapata vipigo hivyo hivyo. Lakini kisheria na kwa sababu sisi tuko ndani ya Baraza la Wawakilishi hatuwezi kuwazuia wao kwenda nje ya Zanzibar kwenda kwenye mashindano ambayo yanafadhiliwa na kitu chochote chengine ambacho hapa tumekikataa ufadhili. Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa hapa kwetu sisi sheria zetu zinatutawala na kutudhibiti ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mchezo wa *boxing* ulikatazwa kupitia Sheria ya Baraza la Mapinduzi kwa sababu Baraza la Wawakilishi lilikuwa halipo na ni kweli ilitamkwa rasmi na hadi leo hiyo sheria bado haikufutwa, kuna sheria kadhaa ambazo zilipitishwa wakati huo ambazo hadi leo zipo hazijafutwa bado na Baraza hili la Wawakilishi. Sisi hatuendi kinyume na tunamuenzi Mzee wetu. Kwa hivyo, hatuwezi kwenda kinyume na sheria hizo, ila kama wawakilishi watahisi kuna haja ya mchezo huu kufanyika, naamini hoja hiyo inaweza kuletwa hapa ikajadiliwa na kama itakubalika na wote hilo suala la sheria hiyo litafutwa.

Lakini mpaka sasa hivi sisi tumeona kama serikali hakuna haja ya sheria hiyo kufutwa ila narudia tena kwamba vijana wale wanapokwenda kucheza huwa wanakwenda nje ya Zanzibar na ndio maana kama serikali kwa kuwa haujaruhusiwa huo mchezo hapa hata sisi wenyewe hatujui mazoezi yao wanafanyia wapi, lakini wanapokwenda hatuwasindikizi rasmi wala kuwapokea rasmi kama tunavyofanya michezo mengine.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, juzi Jumapili nilikuwa

nasikiliza redio ya *Zenj FM* alilolaumu Mhe. Said Ali Mbarouk humu katika Baraza wakati akichangia Mswada wa Tume ya Utangazaji alilaumu redio hii kwa kutangaza pombe, lakini wakati wa kujibu mapigo akasema kwamba sisi wawakilishi tunakataza jambo ambalo tunalifanya. Na akatoa ushahidi kwamba wametushuhudia katika timu yetu na Bunge wawakilishi wetu wakivaa jezi za *TBL*. Kwa hivyo, akauliza swali kwa nini wawakilishi mnakataza jambo ambalo nyinyi wenyewe mnalifanya? Sasa kwa mantiki hiyo na mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri.

Je, ikiwa vyombo vya utangazaji vimetuona kwamba tunavaa jezi za *TBL* na sisi tunakataza mambo haya ndani ya nchi, majibu haya ya redio hii yana ukweli, na kama yana ukweli tutajirekebisha vipi katika Baraza.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli *Zenji FM* walizungumza hivyo Jumapili hata mimi walinipigia simu kutaka kuni-*interview* juu ya suala lile lile kwa sababu wao wanashiriki. Wamejikubalisha kwamba wanashiriki katika kutangaza pombe na sigara na kama jibu nilivyolitoa awali wakati tunazungumzia Tume ya Utangazaji nikatoa mfano wa maadili ya mtu mwenyewe hata katika hoteli yake. Nikachukua mfano wa Hoteli ya Mazsons, pia nikachukua na mfano wa *Tembo Hotel* na jinsi wao walivyoamua kwa maadili yao wenyewe binafsi.

Lakini suala hili la Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuvaa fulana hizo hilo si kweli Mheshimiwa, labda walikuwa wanalitumia kwa vionjo tu na kwa kweli wanatakiwa waliombe radhi Baraza la Wawakilishi kwa kuwasingizia Wawakilishi wa wananchi kwamba wao badala ya kuonesha mfano mzuri wao wakiwa wamevaa fulana hizo za pombe. Kwa hivyo, tunawataka kama wizara, *Zenji FM* kuomba radhi Baraza pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi haraka iwezekanavyo kwamba hawakuvaa na kama walivaa basi walete ushahidi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 21

Ligi ya Majimbo

Mhe. Haji Mkema Haji - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibu kumeanza rasmi Ligi za Majimbo kwa shindikizo la serikali. Je, kwa nini wizara haifanyi bajeti ya kuendesha ligi hizo badala ya mzigo wa gharama hizo kutupiwa Wabunge na Wawakilishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa si kweli kwamba serikali ama Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imetoa shindikizo lolote la kuanzisha wala kubuni mashindano hayo ya majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa mwaka 2009 yamefanyika mashindano ya ligi ya majimbo na kufanyika kwa ligi hiyo ya majimbo hakutokani kabisa na shindikizo lolote la serikali wala wizara yetu ya habari. Kwa sababu tayari mwaka 2008 mashindano ya majimbo yalikwishaanzishwa na majimbo yenyewe, yakishirikiana na kamati maalumu ya Chama cha Mchezo wa Mpira wa Miguu (*ZFA*), ambapo wao majimbo walikaa pamoja na *ZFA* kubuni na kuja na mashindano hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kilichofanyika kwa upande wa wizara yetu ni kusaidia kuyatambua mashindano hayo na kuandaa utaratibu mzuri wa kuyaendesha mashindano hayo ili yaweze kwenda na wakati na yakubalike hapa nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ufinyu na bajeti ya wizara yetu hasa katika sekta ya michezo ni vigumu sana kuweka bajeti ya mashidano ya majimbo kwenye bajeti ya wizara yetu. Hivi sasa wizara kwa mwaka huu ilipangiwa bajeti ya shilingi milioni mia moja ishirini tu, ambapo mahitaji halisi ya wizara nzima kwa upande wa michezo yote ni shilingi bilioni mbili, na hiyo ni asilimia tano tu pamoja na kushiriki michezo ya kimataifa.

Tunachofanya sasa kwa ufinyu wa bajeti huwa tunafuata wafadhili mbali mbali kama vile *Vodacom, Ocean View, ZANTEL* na wengineo, ambapo hufidia katika ile kasma iliyopungua ya kupata ufadhili au kuendesha michezo moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mashindano hayo yanasimamiwa na majimbo yenyewe pamoja na kamati maalum ya *ZFA,* basi si vibaya kwa Wabunge, Wawakilishi na wananchi katika majimbo kuchangia maendeleo ya michezo katika majimbo yao na kuona kuwa ushiriki wa wachezaji kwenye majimbo unakuwa wa ufanisi na ushindani. Pale watakapoona ni mzigo basi mashindano haya yanaweza kuachwa mkono na yakafungwa kabisa.

Ninachotaka kusema kwa mwaka jana tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj, Dr. Amani Abeid Karume, ambapo alitoa zawadi mwenyewe kuchangia timu hizo moja kwa moja kutoka mfukoni kwake. Tunamshukuru sana na hii ni changamoto moja

wapo aliyotoa katika mashindano haya ambayo yamebuniwa na majimbo pamoja na kamati ya *ZFA*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri, namuuliza swali moja la nyongeza. Michezo ni moja katika mambo yaliyotangazwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa Mhe. Waziri anaposema kuwa kuna ufinyu wa bajeti na sehemu ya michezo ikawa haipatiwi fedha, hivyo kweli anatufanyia haki.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba michezo imo katika sera ya chama, imo kwenye sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, inatekelezwa kwa mujibu wa muongozo wa hizo sera. Lakini katika hizo sera haikuzungumzwa kwamba kutakuwa kuna michezo ya majimbo, kumezungumzwa kutakuwa na michezo ya kitaifa na kutakuwa kuna timu mbali mbali za maeneo mbali mbali kama vile wilaya, mikoa na kadhalika.

Bajeti yetu pamoja na udogo wake imejikita katika yale maeneo ambayo tuliahidi kwenye Baraza hili kwamba tupewe fedha tuendeshe michezo kwa mujibu wa sera zetu tulizozitangaza. Katika suala hili mashindano ya majimbo halimo. Nasema kwamba ilipokuja hoja ya kuanzisha mashindano ya majimbo tuliona ni hoja nzuri na tukasaidia katika kusimamia na kuendesha, lakini hivi sasa kuna mashindano mengi tokea *league* ya *ZFA* kusita, kuna mashindano mbali mbali yanayofadhiliwa na wenyewe wanaoyasimamia mashindano hayo.

Majimbo yamesimamia vizuri mashindano yao, hawakuja serikalini kuja kuomba senti hata moja. Kwa hivyo, analolizungumza Mheshimiwa aliyetoa hoja hii sina hakika kama ni sahihi. Usahihi ni kwamba, wakija kutuomba pesa, pesa hizo tutazileta katika Baraza la Wawakilishi tutasema pesa hizi tunazihitaji kwa sababu gani na tukizipata tutawapa majimbo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, Waswahili wana msemo wanasema, "mtoto akiomolea huwa anaomolea wazee wake". Wakati serikali imeandaa kama mashindano ya majimbo imekubali kuwa majimbo yafanye mashindano ili kukuza vipaji vya wachezaji wetu na kupata motisha kwa wachezaji wa nchi yetu. Sasa hivi tayari mashindano ya majimbo yameshaanza na hapa mtoto ameomolea na mzee ni serikali.

Je, Waziri haoni kama kuna haja ya serikali kuyaandaa mashindano yale ya majimbo na ikasimamia na kuwahudumia ili kukuza vipaji vya wachezaji wetu.(*Kicheko*)

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana namuomba Mhe. Subeit Khamis Faki anitafsirie neno 'kuomoa' maana silijui. Kwa hivyo, anitafsirie ili nipate kujibu hilo swali.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kuomoa ni kwamba mtoto akifanya kitu yaani kama atafanya hasara au jambo jema lile analolianzisha basi huwa anaanzisha kwa kuwa anajua kuna mzee atamsaidia huku nyuma. Kwa hivyo, na watu wa majimbo wameanzisha hicho kitu, sasa serikali isaidie.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumwambia Mhe. Subeit Khamis Faki kwamba wakileta rasmi maombi hayo hiyo kamati ya majimbo pamoja na kamati ya *ZFA* kwa pamoja basi serikali sisi tutalipokea na tutaliwasilisha kibajeti hapa Barazani na bajeti ile itapopitishwa basi kule kuomoa kwa mtoto kutakuja humu ndani.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali la nyongeza:-

(a) Kwa kuwa mashindano haya ya majimbo yanashirikisha wachezaji ambao hata timu zao wengine haziko kwenye *league* na ukiangalia kwenye *league* huwaoni. Je, haionekani kuwa kuna haja ya mashindano haya kutumiwa pia katika kutafuta wachezaji wa Timu ya Taifa ya Zanzibar.

(b) Pamoja na mashindano haya, pia kuna makombe kadhaa kama vile kombe la Marehemu Thabit Kombo, kombe la Mapinduzi. Je, makombe haya nayo mashindano yake, mipaka yake ni mpaka wapi. Ikiwa mipaka yake inavuka Zanzibar hatuoni kwamba kombe hili likichukuliwa nje ya Zanzibar itakuwa ile ladha ya lile kombe ndani ya Zanzbar itapungua.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa utaratibu ambao huwa wanapanga hawa wa majimbo wenyewe katika hizi ligi zao wana usajili wao maalumu. Tatizo hili hata mimi kwa jimbo langu liliwahi kutokea kwa sababu jimbo lilitaka kushinda. Nakumbuka timu zilizokuwa zikitamba ilikuwa Kikwajuni, Kwahani, Fuoni na Chumbuni. Hayo ndio majimbo yaliyokuwa yakitamba hapa kwetu mjini. Sasa katika ile timu yangu wao wakataka kuchukua mateka, sasa walipotaka kuchukua mateka kutoka timu kubwa *ZFA* ikawakatalia kwa sababu walipanga utaratibu wao maalumu wa usajili kwa ajili ya majimbo. Utaratibu huo ni wao wanaopanga *ZFA.*

Ingekuwa vyema sana wangepanga hata umri kwamba wangechukua wachezaji chini ya miaka 17 ili tukapata kuibua vipaji vingi zaidi. Lakini hilo hawajalipanga na tutajaribu kuzungumza nao ili waliangalie hilo kwa karibu sana.

Upande wa pili umeuliza kuhusiana na makombe haya mengine kama vile Kombe la Mapinduzi na Kombe la Thabit Kombo. Kombe la Mapinduzi lilijumuisha timu kutoka Tanzania Bara kwa sababu kuna washabiki wengi, hata humu ndani ya Baraza timu kama Yanga na Simba. Hili lilijaribu kushajiisha yale Mapinduzi yenyewe kama yanavyofanyika makombe mengine ya Uhuru wa Tanganyika, huwa wanatualika timu zetu tunakwenda kucheza kule kwenye sherehe zao pamoja na sherehe nyengine za Pasaka na kadhalika.

Lakini kweli inatuuma sana pale kombe ambapo hutoka Zanzibar na safari hii limetoka pale katika Uwanja wa Gombani Pemba ilituuma sana, hata katika ushangiliaji haukuwa mkubwa kwa sababu lile kombe limetutoka mikononi mwetu limekwenda kwa wenzetu Tanzania Bara. Lakini nia kuu na lengo ni kushajiisha.

Ukitizama kama hili kombe la Thabit Kombo limejaribu sana kuchukua timu za ndani ya mipaka ya Zanzibar ikiwemo Timu ya Jamhuri ya Pemba ambayo nasikitika sana kusema kwamba ilitolewa mapema mno. Tulikuwa tukiitegemea kufika mpaka mwisho, lakini hili limejumuisha zaidi timu za Zanzibar na timu za madaraja mbali mbali kama *FA* inavyofanyika Uingereza *FA Cup,* huwa inachukua daraja la kwanza *premier*, daraja la pili na kadhalika. Kwa hivyo, hili tumechukua kiujumla yake.

La tatu, hivi sasa tuna mfadhili mmoja ambaye yeye hasa anataka kuibua vipaji. Kama itafahamika au kukumbukwa timu yetu ya Kopa Cocacola ambayo ilituletea ushindi mkubwa hapa mara moja na ile timu ya Mkoa wa Mjini Magharibi ambayo pia iliwasilisha zawadi hapa Baraza la Wawakilishi. Timu zile tunataka kuzifanyia *league* zake za watoto wadogo yaani *central* na kuja chini, ambapo ilikuwa inafanyika pia katika kombe la Hija Saleh.

Kombe la Hija Saleh nimeangalia vijana wa rika kuanzia miaka 17 au 15 kuja chini. Sasa kwa kuwa mfadhili huyo tumempata na yeye hasa amekuja kuibua vipaji na anataka kuvichukua kutoka Zanzibar kuvisafirisha kwenda nje kwa ajili ya mchezo wa kulipwa basi tunatarajia hivi karibuni tutaanzisha *league*. Isipokuwa kwa timu za Pemba, natoa wito timu za watoto wadogo kwa sababu sijui *central league* sijaiona bado ya Pemba, nimekwenda mara kadhaa, lakini bado sijapata ule mfumo wao wa *central* na *junior* na *juvenile* ambayo ni madaraja ya chini.

Wawakilishi kutoka Pemba wangetusaidia sana kushajiisha kule ili timu za Pemba nazo ziweze kushiriki katika mashindano haya, huenda tukaja kufanyia mashindano hayo Pemba Gombani kwa sababu hapa bado Kiwanja cha Amani kinatengenezwa, na kutokana na mfumo huo tungependa kuchezea Kiwanja cha Gombani Pemba. Ingawa ni gharama kubwa kusafirisha timu zote kutoka Unguja kwenda Pemba lakini mfadhili amekubali kulipokea hilo na tutaendelea kulifanyia kazi. Lakini wawakilishi tunawaomba sana watusaidie kwa timu zile za watoto wa Pemba.

Hivi karibuni tulisikia kuna kombe la Mbunge wa Wawi. Kwa hivyo, hilo kombe lilishirikisha timu ndogo. Tulisikia habari zake na tunalifuatilia kwa karibu sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Baraza la Wawakilishi ni Baraza tukufu na lina Wajumbe watukufu, sasa pametoka kauli hapa kwamba Baraza la Wawakilishi timu yetu ya Baraza la Wawakilishi wachezaji wetu walivaa jezi zenye alama ya pombe. Hiyo ni kashfa kwa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri alisema wizara yao imewataka hao waliofanya mambo hayo waombe radhi. Sasa naagiza wadhamini wetu humu ndani washirikiane na Afisi ya Baraza kuhakikisha hao waliofanya hivyo waombe radhi kwa maandishi.

Nam. 17

Mitaala kwa Skuli za Serikali na Watu Binafsi

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatarajia kuweka mtaala (*Curriculum*) wa elimu unaolingana baina ya Skuli za Serikali na skuli za watu binafsi mapema mwakani na kwa kuwa wanafunzi wa skuli hupangiwa mitaala kulingana na uwezo na umri wao.

Mhe. Waziri, Wizara yako itakuwa na mpango gani maalumu kuhakikisha kwamba skuli za binafsi zinafuata mtaala huo wa taifa bila ya kuongeza masomo ya ziada kinyume cha mtaala huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wizara yangu imeandaa mitaala mipya ya Elimu ya Maandalizi na Elimu ya Msingi kwa ajili ya kufundishia katika skuli zote zilizopo Zanzibar. Mitaala ya Elimu ya Maandalizi ilianza kutumika kwa majaribio mwaka jana na mtaala wa Elimu ya Msingi ambao uliandaliwa mwaka jana utaanza kutumika rasmi kuanzia mwaka huu kwa kuanzia na wanafunzi watakaoingia darasa la kwanza mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, mitaala hiyo imeandaliwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006 ambapo elimu ya maandalizi itatolewa kwa muda wa miaka miwili na elimu ya msingi itatolewa kwa muda wa miaka sita.

Mhe. Mwenyekiti, skuli zote za maandalizi na msingi za serikali na binafsi zinapaswa kufundisha kwa kutumia mitaala mipya na pindipo skuli za binafsi zinataka kuongeza baadhi ya mada au masomo wanapaswa kuomba kibali kutoka Wizara ya Elimu.

Wizara itahakikisha kuwa skuli zote zikiwemo na skuli za binafsi zinafuata mtaala huo. Mihutasari hiyo itasambazwa katika skuli zote za serikali na za watu binafsi ikiambatana na Toleo Maalumu la kusisitiza skuli zote kutumia mitaala hiyo. Aidha, Wakaguzi wa Elimu na Maafisa mbali mbali kutoka wizarani na idara watazipitia skuli zote ili kuhakikisha kwamba mihutasari hiyo inatumika.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, swali linazungumzia mitaala, tunapozungumzia mitaala inajumuisha mihutasari, vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia. Naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri. Je, mambo yote hayo ya mitaala tayari yameshapatikana? Kama hayajapatikana kwa mujibu wa ratiba ya wizara ni lini mahitaji ya mitaala hii yatakamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba swali alilouliza linahusu mambo ya mitaala, ambayo inaingiza mambo ya vitabu, mihutasari na mambo mengine kama alivyosema.
Mhe. Mwenyekiti, napenda niseme kwamba tayari wizara imeshaanza maandalizi ya kuhakikisha kwamba mambo yote hayo yanapatikana wakati tunatekeleza sera yetu hii ya elimu ambayo tumeipitisha mwaka 2006.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu swali hili aliegemea upande mmoja tu wa skuli za msingi. Sasa nataka kujua kwa upande wa skuli za sekondari ni hatua ipi wanayochukua kuhakikisha kwamba ile mitaala inayopaswa kufundishwa kwa mwaka ule ndio hasa inayofundishwa kwa skuli zetu za serikali na skuli binafsi.

Labda atueleze kwa mwaka huu kuna tatizo gani kuhusiana na hasa somo la hesabu, wenyewe wanaita hesabati.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Ni kweli kwamba nilipokuwa najibu swali mama nilihusisha zaidi suala la elimu ya msingi na suala la elimu ya maandalizi. Lakini napenda nimhakikishie kwamba hata katika elimu ya sekondari tunachukua hatua ya kuona kwamba mitaala inayohusika ndio ambayo inafundishwa. Hili huwa tunazikagua skuli zote ambazo zinafundisha mitaala hiyo na pale inapoonekana kwamba skuli haifuati mtaala huo basi hatua na taratibu huwa zinachukuliwa.

Kuhusu tatizo la mwaka huu kwa somo la hesabati. Ni kweli kwamba kulikuwa na matokeo ya mtihani mwaka huu kuhusu somo la hesabati sio mazuri kiasi hicho, lakini wizara inafanya jitihada ya kufanya utafiti kuona kwamba kwa nini mwaka huu na miaka ijayo pengine kama matokeo haya yatakuwa mabaya. Tayari tumeshawaelekeza maafisa wetu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Zanzibar kuona kwamba wanafanya utafiti kuhusu suala zima la tatizo la hesabu hapa visiwani.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Hapa kuanzia mwaka 2012 Wizara ya Elimu inataka kuhakikisha kwamba mwanafunzi wa darasa la kwanza hatochukuliwa mpaka apitie skuli ya maandalizi. Kwa bahati mbaya sana skuli nyingi hazijaweka utaratibu wa kuandaa skuli za maandalizi. Pamoja na kuwa kwamba wizara yake inatumia redio wanaita elimu kwa njia ya redio. Hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri hapo itakapokuwa tayari zoezi hili limekamilika.

Je, kwa zile skuli ambazo hazijawa na skuli za maandalizi zitachukuliwa vipi. Na kama utaratibu utakuwa umewekewa mkazo, haoni kwamba baadhi ya maeneo mengine wanafunzi wa darasa la kwanza hawatopatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wizara yangu imeandaa sera mpya ya elimu na suala zima la maandalizi ni moja ya mambo ambayo yametiliwa mkazo katika sera hiyo na imeelekeza skuli mbali mbali kuanza utaratibu wa maandalizi ya kuitekeleza sera hii. Tayari tumeshawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kushirikiana na wananchi kuona kwamba sera hii inafanikiwa au inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, kufanikiwa au kuanza kwa sera hii itategemea zaidi mashirikiano makubwa yaliyopo baina ya wizara na wananchi wenyewe

ambapo wananchi wanatakiwa washiriki kikamilifu. Nadhani hakutakuwa na mtu ambaye ataachwa kuingia darasa la kwanza kwa sababu hakuanza maandalizi, lakini nadhani itakapofanikiwa kwa maana ya kwamba skuli zote tayari zitakuwa zimeshatekeleza mpango huu, hapo ndipo ambapo tutasema sasa hivi tunaingia katika mpango huu. Lakini kama bado kuna baadhi ya skuli ambazo hazijaanza, nadhani tutasisitiza kwamba zianze na ziweze kuona kwamba sera hii imefikia pahala.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la pili alizungumza kwamba itakapofika hapo ambapo tutakuwa tumeanza kwamba kuna skuli nyengine hazijakuwa tayari. Nadhani hatutoanza kama skuli nyengine hazijakuwa tayari, lazima skuli zote ziwe tayari ili kuhakikisha kwamba sera hii inafanikiwa. Hili tutajitahidi kushirikiana na Kamati za Skuli pamoja na wazee kuona kwamba sera hii inafanikiwa.

HOJA ZA SERIKALI

Sera ya Nishati Zanzibar

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunijaalia asubuhi hii, Mwenyezi Mungu akakuongoza unianzie kunipa ruhusa pamoja na kuwa jana ulisema ataanza Mhe. Said Ali Mbarouk, lakini naona nyota yangu kali zaidi kuliko yake.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaingia ndani ya sera hii, naomba kwanza nisiwe mwizi wa fadhila nitoe shukrani. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nitoe shukrani kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa Mwenyezi Mungu kumpa *ilham* amteue Mhe. Mansoor Yussuf Himid kuwa Waziri wa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, pili pia nitoe shukrani na pongezi kwa Mhe. Mansoor Yussuf Himid mwenyewe aliyeteuliwa kwa kazi nzuri anazozifanya katika wizara hii na mpaka leo ikawa tunajadili mambo mazito ya maslahi ya taifa hili. Kwa kuanzia naomba nitoe shukrani hizo na nyengine, kwanza niziahirishe mpaka wakati wake utakapofika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna athari kubwa sana katika matumizi ya nishati. Athari hizi ndani ya sera hii zimeelezwa na wachangiaji wengi wamezitaja. Sasa kutokana na athari hizo ni dhahiri kuwa kulikuwa na haja ya kuwa na Sera hii ya Nishati, ili itafutwe njia ya kuzipunguza na ikiwezekana kuziondoa kabisa athari hizi ambazo zinawapata watu wetu hasa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, ninapozungumzia athari hizi kwa wanawake na watoto, huwa nakumbuka mengi yanayotokea vijijini. Mhe. Mwenyekiti, wanawake na

watoto ndio wanaokwenda misituni kutafuta kuni. Mhe. Mwenyekiti, wanawake na watoto hasa wa kike ndio wanaokaa jikoni kupika. Mhe. Mwenyekiti, katika kupika wanawake na watoto huungua, ukiachilia mbali moshi mwingi wanaoumeza kila siku haipungui mara tatu, asubuhi, mchana na jioni. Ninahakika kuwa miongoni mwa matatizo ya kiafya wanayoyapata wanawake na watoto mengine yanachangiwa na athari za nishati hizi ambazo zinatumiwa kwa wingi sana sasa hivi.

Watu walitarajia kuwa wakitumia makaa, samahani naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu jina hilo ndio nililokulia nalo la makaa na sio mkaa. Watu walitarajia wakitumia makaa watapunguza lile tatizo kubwa linaloletwa na kuni la moshi. Lakini nikuthibitishie Mhe. Mwenyekiti, kuwa makaa ya hivi sasa hayaivi, matokeo yake yanapotiwa kwenye maseredani yakawashwa huwa kuna moshi utafikiri unapikia kuni. Haya yananipata hata hapa hapa ninapokaa, wakipika tu jirani zangu basi moshi unakuja ndani na wanatumia makaa, hawatumii kuni.

Kwa hivyo, bado lile lililotarajiwa kuwapunguzia matatizo ya afya wanawake na watoto halijawa na ukitilia maanani kuwa jamii yetu ni jamii ya watu maskini. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katwambia kuwa katika utafiti uliofanywa wa pato la kila mtu limesimama kwenye shilingi 639,000 kwa mwaka ambalo hilo ni sawa na shilingi 1,775 kwa siku. Ninalotaka kusema katika hili Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa hili ni pato la nadharia ya kiuchumi. Maana yake wamechukuliwa wanaopata shilingi milioni 2 na 3 kwa siku wakachanganywa na wanaopata shilingi 102 kwa siku, baadae ikatafutwa wote kwa pamoja ingekuwa pesa zile ni za jumla pamoja wakagaiwa watu wote zingekuwaje, ndio zikapatikana hizi.

Lakini katika hali halisi Mhe. Mwenyekiti, watu wanapata pato dogo sana kuliko hili. Kwa maana hiyo, nishati zilizopo hivi sasa zinawafanyia matatizo kubadilisha kutoka nishati moja kwenda nishati nyengine kutokana na umaskini wao, ukiachilia mbali lile lililozungumzwa la mazoea. Kweli wapo waliokuwa wanaogopa kwa mazoea, pia wapo wanaotamani wafanye yale mazuri lakini uwezo hauwaruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kidogo niende sasa hivi katika sera yenyewe. Katika sera nataka nianze na tamko la kwanza ukurasa wa 19 katika sehemu ya mikakati. Hapa kunaelezwa mambo mengi kuhusiana na tamko hili jinsi gani litakavyotekelezwa. Lakini kuna kitu kimoja muhimu sana ambacho nadhani hakikutajwa na kingestahiki kutajwa katika mikakati.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tuna wafugaji wengi sana. Pemba hatuagizii ng’ombe na kila siku wanaliwa ng’ombe sijui wangapi. Hii maana yake ni

kuwa kuna wafugaji wengi sana na kuna ng'ombe wengi sana Unguja na Pemba. Wanyama hawa kama watatumiwa vizuri wanaweza wakatoa nishati ya gesi inayoweza kutumiwa na mfugaji mwenyewe.

Lakini kutokana na kutokuwa na elimu ya habari hizo, kutokana na kutokuwa na uelewa wa mambo hayo, wafugaji wengi hawana mazizi ya kuweka ng'ombe wao. Ng'ombe wanalala misituni, wanaamka misituni, kubwa ni kwenda kufungwa asubuhi, mchana akageuzwa na usiku akatafutiwa pahala pengine akawekwa.

Katika hali hiyo tunakosa mambo mawili muhimu, tunakosa nishati inayoweza kutokana na kinyesi cha ng'ombe hao, lakini pia tunakosa na mbolea ambayo ingetumika katika kilimo. Kwa hivyo, nadhani kuna haja hapa kuingizwa mkakati mwengine wa kuwafundisha wananchi walio na mifugo jinsi ya kutengeneza nishati ya gesi kutokana na kinyesi cha mifugo yao na ikawasaidia nishati hiyo kuitumia katika shughuli zao mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika hoja ya 6 ya sera juu ya ukadiriaji wa bei za muda mrefu za umeme. Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Mjumbe mmoja alizungumza lakini hakufafanua alisema "Nguo ya kuazima haiendewi ngoma au haistiri". Lakini mimi nataka kidogo hapa nieleze ilikuwaje mpaka ikataja methali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu, siku moja kuna mtu alikuwa anataka kwenda ngoma, lakini hana nguo nzuri ya kuvaa itakayomfaa kwendea kwenye ngoma na yeye akawa kama wenzake. Kwa hivyo, akenda kwa jirani yake kuazima nguo ya kuvaa anakwenda kwenye ngoma. Akaomba ile nguo, lakini akaomba kwa masharti, kuwa naomba nguo, lakini usije ukaniadhiri bwana, tena nimeshachukua nguo yako tukifika kule ukaja ukaniadhiri. Akamwambia hilo sifanyi hata siku moja sithubutu, nguo chukua vaa nenda zako kwenye ngoma. Akavaa nguo ile akenda zake kwenye ngoma akasimama akatazama ngoma.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mdundo ulipokolea alishindwa kusimama akatazama ngoma, ilibidi aingie aanze kucheza ngoma. Kacheza ngoma katipuka, katipuka, nguo zinamroa jasho, mwenye nguo akaona aaa sasa nguo yangu ananiharibia. Alimwambia wewe cheza nayo tu hiyo, sikuulizi habari ya nguo. Basi mdundo ukazidi mpaka ikabidi agaregare chini. Akamwambia garagara tu wewe nguo hiyo haina tatizo nitafua mimi. Mhe. Mwenyekiti, yale aliyoyakataa ndio aliyoyapata.

Sasa kwa kuwa nguo ya kuazima haiendewi ngoma, umeme huu tunaoupata na tutakaoupata huko Pemba tusije tukauendea ngoma kwa sababu kitu chochote kiangalie kinavyokwenda. Watu wanasema “Dalili ya mvua ni mawingu”.

Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa ndani ya Baraza hili kwamba umeme ulipopandishwa bei Bara na *EWURA*, wao wenyewe walijipendelea wakajipandishia kidogo asilimia 21. Lakini sisi waazima nguo wakataka kutupandishia asilimia mia moja sijui na sitini na ngapi, sasa hii ni nguo ya kuazima ndio kawaida yake ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi hicho kilichopita baada ya mizozo mirefu mpaka ikafika Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akaingilia kati jambo hili likapoa. Lakini ninavyodhani upoaji huu si upoaji halisi ni upoaji wa kigaga, kuna siku kigaga kitabanduka kidonda kitakuwa bado kipo. Mhe. Mwenyekiti, samahani. Kwa hivyo, wakati huo hatujui kitaibuka vipi kuwa kitakuwa vile vile kidogo au kitakuwa jeraha kubwa la kuhitaji mtu kuchunwa na kubandikwa ngozi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo linapozungumziwa suala zima hili la kurekebisha bei za umeme ziwe za kudumu za muda mrefu na zitakazowezekana na wananchi, basi nadhani kuna haja ya kuwa na mikataba madhubuti na pia kuwa na nia ya kuwa hiki ni kipindi cha mpito. Isije ikawa watu husema “Mke wa mshikizo”, lakini isije ikawa ni mshikizo na mke kabisa. Hili ni moja katika jambo ambalo ningelipendelea sana nilizungumzwe na Mhe. Waziri, aliangalie jinsi gani atalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya sera ya 15 katika mikakati uandikaji wake naona imetofautiana na wenzake. Sasa labda niseme tu mkakati wa kwanza umeanzia na “Anzisha Modeli”, mkakati wa pili “Anzisha na kufanyia Mpango”, mkakati wa tatu “Hamasisha”, mambo haya anaambiwa nani. Mikakati yote niliyoisoma nyuma imesema kufanya mapitio, kukuza uanzishaji, kupitia kanuni, haikutoa amri lakini hii imetoa amri.

Sasa pengine katika utaalam wa sera inawezekana kuna baadhi ya mambo huelezwa vyengine na baadhi ya mambo hutolewa amri. Ingawa kwa mawazo yangu basi vyovyote itakavyokuwa kuwe na uwiano *(uniformity).* Ikiwa tunatoa amri basi mikakati yote tutoe amri, ikiwa tunatoa maelezo basi mikakati yote tutoe maelezo. Hili ni jambo jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nahitaji nilieleze.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Wajumbe waliozungumzia hapa umeme wa *solar* katika visiwa. Hili naomba Mhe. Waziri alifanyie kazi zaidi ili visiwa vyote

vipate huu umeme wa *solar* kwa sababu hivi sasa visiwa vyengine tayari vimeshaanza kuona choyo.

Mimi nilipokwenda Makoongwe hivi karibuni wananambia “Mheshimiwa vipi sisi mbona hatujapata umeme wa *solar*, kuna visiwa vimeshapata”. Nikawaambia mambo yanakwenda kidogo kidogo na nyinyi mtapata *inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri ili hii hamu ya maendeleo waliyonayo visiwa mbali mbali vidogo vidogo iweze kutoshelezeka, basi hili nalo angelifanyia utaratibu wa haraka kidogo wakaweza kuburudisha nyoyo zao.

Mhe. Spika, nije kwenye mafunzo. Kwa kweli ni vyema watu kupelekwa kwenye mafunzo. Nafurahi sana, nashukuru na nampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi zake alizozifanya mpaka zikapatikana nafasi mbali mbali za mafunzo watu waende wakasome. Lakini linalokwenda kusomwa hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, katika masuala mazima ya nishati ni suala la mafuta. Nishati sio mafuta tu, tuna vyanzo mbali mbali vya nishati. Mhe. Mwenyekiti, hapa napendekeza kwa Mhe. Waziri kuwa wakati anatumia nafasi hizi kuwapeleka watu kwenda kujifunza, wakati huo huo atafute na nafasi nyengine za watu kwenda kujifunza aina nyengine za nishati, ili watakaporudi wawe ni walimu wa kuja kushughulikia na kufundisha mambo ya nishati nyengine, kuzitayarisha, kuzipata na kuzitumia.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa katika suala la mafunzo, naomba niungane na Mhe. Haji Faki Shaali kusema kuwa “Mcheza kwao hutunzwa”. Kwa hivyo, wale wanaocheza mpaka wakalifikisha hapa nao wasije wakaachwa ikiwa sifa za kwenda kujifunza wanazo.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la uchimbaji wa nishati ya mafuta, mafuta hayatoki mafuta peke yake, katika kuya-*process* mafuta huwa kuna na vitu vyengine wenyewe wanaita *by product*, kwa mfano lami. Sera hii haikusema *by product* zitakazotokana na nishati zitafanywa nini. Kwa hivyo, naomba na hilo liingizwe katika sera kuwa kama kutapatikana mafuta *by product* zake je, zitafanywa nini, ili litakapotokea suala hilo basi isije ikawa kuna tatizo tena la kujiuliza haya hii lami sasa tuifanye nini, au hili jambo jengine tulifanye nini.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyotangulia kusema Mhe. Haji Faki Shaali kuwa likitangulia zumari basi kinanda huwa hakina tena hadhi na mchangamsho. Naomba nimalizie kwa kusema natoa shukrani kwa watendaji wote wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kazi nzuri wanazozifanya na kwa kazi hii waliyoifanya ambayo tumekuwa tukiijadili. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Ali Salim huna zaidi.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, zaidi niliyonayo ni kuwa naunga mkono hoja.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya mwisho kabla ya Mhe. Naibu Waziri na Waziri wake katika kukamilisha mjadala huu wa hoja. Kwa kweli kama tulivyokubaliana nitachukua muda wa dakika kama 10 hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mambo yangu ni manne. La kwanza, naomba nisisitize kwanza kuwapa pongezi Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutuletea *document* nzuri ambayo kwa kweli inaonekana inakamilika sana.

La pili, ni suala la sera hii utamu wake na uzuri wake unahitaji idara madhubuti ya kuisimamia, kwa inavyoonekana lazima labda iwe Idara ya Nishati. Sasa mimi naomba nisisitize suala la Idara ya Nishati kuipa mafunzo, inahitaji mafunzo makubwa na kuimarishwa ili iweze kuisimamia hii sera kwa niaba yetu. Ilivyo leo Idara ya Nishati sijui, lakini mimi niliwahi kufanya kazi wizara hii na nilikuwa Pemba. Idara ya Nishati enzi hiyo nafanya kazi ilikuwa na mtu mmoja tena wa darasa la nane, ndie aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Nishati, yeye akicheza, akipiga, akiimba, huyu huyu mtu mmoja.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa majukumu ya hii sera ilivyo, idara hii inahitaji kuimarishwa sana kimafunzo, kimaslahi, fursa za kujifunza nyengine na mambo mengine. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri wakati anafanya matayarisho mengine, suala hili ni muhimu sana. Kwa wenzetu ukenda katika Idara za Nishati utaona kwa kweli hawa watu wako makini. Naamini kuwa umakini umeanza basi na hili Mhe. Waziri atalipa kipaumbele sana. Tunahitaji kwa kweli Idara ya Nishati ambayo ukenda mle utakuta mtu ambaye ana taarifa za *wind power*, *solar power*, *wave power* kwa mazingira ya kisiwa chetu. *Atleast* upate mtu ambaye ni *conversant* wa mambo haya, huwezi kwenda pale ukasema sisi mambo haya hatujui bwana.

Kwa hiyo, tulikuwa tunahitaji Idara ya Nishati iliyokamilika, tunahitaji Idara ya Nishati ambayo inamiliki *experiment station* moja au mbili kuangalia mambo, hatuwezi kuwa na Idara ya Nishati ambayo haiko hivyo, hiyo ni muhimu.

Lakini pia, tunaangalia suala la uchimbaji wa mafuta. Tunahitaji idara ambayo itakuwa mwenyeji wa makampuni yatakayokuja kutoka nje. Wenzetu wa Kenya wanayo *National Oil Company of Kenya*, Uganda wanayo idara lakini inajitegemea katika suala hili. Tanzania Bara wana *TPDC*. Kwa kweli na sisi

tunahitaji kampuni itakayokuwa inajitegemea ambayo itakuwa ni mwenyeji wa makampuni ambayo yanatoka nje.

Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri hili alipe kipaumbele kikubwa. Kama walivyosema wenzangu kwa wale ambao wapo, lakini hivi sasa wanahitaji kupewa motisha, kupewa ahsante na kwa kweli wawe wenyeji wa vijana wapya watakaokuja.

Kuhusu suala la sera, mimi naomba nizungumzie mambo mawili ambayo sikuyaona katika hii sera. La kwanza ni suala la *conflict resolution*. Tunapochimba mafuta, tunapochimba gesi suala hili ni mambo ya kawaida sana katika nchi hasa za Kiafrika. Tumeona wenzetu ambao wameingia katika suala la uchimbaji wa mafuta na gesi, lakini suala la utatuzi wa migogoro hawakujiandaa mapema. Bahati mbaya nimeisoma hii sera haraka haraka, lakini sikuona eneo ambalo suala la utatuzi wa migogoro limepewa nafasi. Kwa hivyo, mimi ningeomba kwamba tutafutiwe utaratibu ambao katika sera hii itaelekeza hasa kwamba namna gani migogoro ikitokea itaweza kutatuliwa.

Lakini suala la pili, ni ugawaji wa keki itakayotokea na hasa katika maeneo ambayo fursa hii itatokea. Kwa mfano kama Chwaka itatokea gesi Halmashauri ya Wilaya ya Kati haiwezi hata kidogo kuona kwamba matangi ya gesi yanasafirishwa kutoka Wilaya ya Kati, huku Wilaya ya Kati haifaidiki na lolote kutokana na mauzo ya gesi inayotolewa. Kwa hivyo, ni lazima sera ielekeze kwamba angalau asilimia ndogo ya *resource* inayouzwa irudi katika Halmashauri ya Wilaya kusimamia shughuli za kimaendeleo za wilaya ile. Bahati mbaya sera hii Mhe. Mwenyekiti haikueleza hivyo.

Kwa hivyo, mambo hayo mawili, la kwanza utatuzi wa migogoro na pia kuwacha chochote katika eneo ambalo rasilimali hii itatokea ni jambo la msingi na hii itasaidia sana katika kuona kwamba wenyeji wanafaidika na lile jambo ambalo linatokea.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali limepewa majukumu, lakini ningeomba niseme jambo jengine ambalo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walifanye ni suala la uundaji wa ndani wa vifaa ambavyo vinatumia ama jua au upepo. Ni aibu kuwa tuna *technical college* na siku hizi kwa sheria tulioipitisha imegeuka *technical* labda *university.* Pia, tuna vyuo vya amali, lakini hatuwezi hata kuunda *windmill* kitu ambacho kinakwenda kwa mbao na *spoke* au nondo ndogo na *dynamo* ambayo inaweza kutia umeme. Sasa mambo kama haya Mhe. Mwenyekiti, yangewezesha vyuo vyetu vilivyokuwa ndani kushajihishwa angalau kuanza kuunda vitu vidogo vidogo hivi ambavyo vingewezesha wananchi kuvimiliki vitu hivi.

Mhe. Mwenyekiti, labda kwa sababu ya muda ulionipa, nizungumzie suala la mwisho la utekelezaji wa sera hii na hasa suala la mafuta linahitaji utulivu katika nchi. Ikiwa nchi haina utulivu Mhe. Mwenyekiti kwa kweli hata tukiwa na nishati ya mafuta ya aina gani, kila pembe ya nchi na kila shehia, kama tuna kisima cha mafuta tuta-*end up* na *violence*, tutauana na hatimaye watu wa nje wa Zanzibar ndio watakaofaidika na nishati hii. Sasa bahati mbaya sera hii haikutaja kwamba kuna umuhimu wa wadau wote kuona kwamba nchi hii ina utulivu wa kisiasa na wa kijamii wa kutosha ili kuwezesha sera hii iweze kutekelezeka.

Bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, sera hii ilipoletwa kumetokea neema hii ya maridhiano ya kisiasa. Sina uhakika wa *sustainability* yake binafsi, naomba iwe hivyo kwamba kuna *sustainability* ya kutosha, maridhiano haya yaendelee vya kutosha ili hatimaye sera hii iweze kutekelezeka kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Lakini katika eneo la wadau wote kulikuwa kuna haja mahususi kuona kwamba wadau wote, hasa wa ndani wana wajibu wa kuona kwamba kuna utulivu wa kisiasa wa kutosha ili neema ambayo itakuja iweze kuleta maslahi na isilete maafa kwa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa na mchango mdogo na nitatumia muda mdogo ili nimpe nafasi Mhe. Waziri na yeye akamilishe kazi ambayo ameianza tokea jana. Kwanza naunga mkono sera hii ambayo imewasilishwa jana hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yamezungumzwa na Wajumbe wako. Kwanza tukipenda au tusipenda hivi sasa na kwa muda mrefu ujao, wananchi wa visiwa hivi tutaendelea kuwa waharibifu wa mazingira, sio kwa kutaka, hali ndio ilivyo. Tutaendelea kutumia makaa na tutaendelea kutumia kuni. Hili hatuwezi kuliepuka kwa sasa pamoja na kuwepo kwa gesi na kuwepo kwa umeme. Hii inatokana na unyonge wetu, wataalamu wanasema ile *purchasing power* ya watu wetu kuwa ndogo. Kwa hiyo, hawamudu kwenda kwenye umeme, umeme tunautumia zaidi kwenye kuwasha taa na sana sana kupigia pasi, tunatumia ma-*cooker* wakati wa skukuu tu, baada ya hapo tunayawacha kwa sababu ma-*cooker* yanatumia umeme mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa Zanzibar kila mwaka nafikiri kuna siku wanaita Zanzibar *solar day*, siku ya umeme wa jua hapa Zanzibar. Maonesho haya mwaka jana nakumbuka yalifanyika hapa Haile Selasie. Kulikuwa na mambo mengi pale yalioneshwa, kulikuwa na majiko yale ya kutumia makaa na kutumia kuni, lakini yanatumia kuni kidogo sana na yanatumia makaa kidogo sana, tena sana.

Mhe. Mwenyekiti, makaa ambayo unaweza ukayachukua kwa mikono hii miwili basi unaweza ukapikia mchuzi, mboga pengine na wali, yanatumia makaa kidogo sana. Hivyo hivyo kuna majiko yanayotumia kuni hazizidi tatu, walionesha pale wakapika wali na vyakula vyengine na mimi nilikula, sikula kwa sababu ya uroho, hapana, nilikula ili nithibitishe kuwa hiki chakula kweli kimeiva. Kwa hivyo, iko haja kwa wakati huu watu wabadilike kutoka kwenye kutumia majiko haya ambayo yanatumia makaa mengi na majiko yetu ambayo yanatumia kuni nyingi, tuende kwenye majiko haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya hapa hajatokea mtu ambaye amekuwa tayari kwenda kuyachukua kule Bara na kuyaleta hapa, lakini yapo. Mimi niliamua ninunuwe baadae. Kwa hivyo, watu tunatakiwa tuende huko. Inawezekana pengine, nasema inawezekana pengine sisi kama wizara ambao tunahusika na mambo ya nishati baada ya kuona maonesho yale pengine hatukuchukua zile juhudi za kuelimisha ile taaluma, nasema inawezekana haya ni mapungufu.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika walipokuja hapa walikuja na *oven* ni *potable* unaweza ukaichukua na kuipeleka pahala pengine, hivyo hivyo inatumia kuni kidogo kwa kuekea mikate. Ambapo kwa wale ndugu zetu na mama zetu waliokuwa wakifanya biashara za mikate hasa ile ya kuumua basi inawafaa sana na itawapa faida kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukizungumza sana hapa juu ya Zanzibar kuwa na chanzo chake wenyewe cha umeme. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili tukipenda tusipende, ingawa sio kufumba na kufumbua, sio leo na kesho, lakini ndani ya ndoto zetu kwenda kwetu hili lazima litekelezeke. Kama tulivyosema kuna njia nyingi na makampuni mengi yanatumia kuna umeme wa jua, umeme wa mawimbi ya bahari na umeme wa upepo. Kimsingi kwa kweli wizara yangu imejitahidi kuwasiliana na makampuni mbali mbali, lakini Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe napenda niseme tu kwamba mimi mwenyewe binafsi katika jambo ambalo nalisimamia mwisho wa uwezo wangu basi ni hili. Takriban kila wiki ni lazima niwasiliane na hawa jamaa juu ya utekelezaji wa mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kidogo ambalo hata jana usiku nilikuwa nikiongea na wale jamaa kule, wamekuwa na hofu kwa sababu kujenga mitambo ya *solar power* ambayo itakuwa na wao walinithibitishia kwamba inawezekana kabisa kuwa na umeme wa *solar power* hadi kufikia *megawatts* 100, waliniambia hilo linawezekana. Lakini kwa sababu gharama zake ni kubwa, wamejenga hofu. Baadhi ya haya makampuni yakawa hayako tayari kuona kampuni nyengine zinapewa fursa za kufanya *study*, kwa sababu wanajua watafanya *study* kwa gharama zake na pengine Sheikh Mazrui pale,

kwa sababu yeye ni mfanyabiashara mjanja mjanja kidogo na yeye anaweza akawa na kampuni, wakaja wakafanya *study* ile. Baadae ni serikali ndio itakayoamua baada ya kutoa taarifa yao, mauzo yatakuaje, ipi mauzo yake yatakuwa na nafuu zaidi kwa wananchi na haitakuwa mzigo, basi ndio itakayopewa fursa na hilo ni lazima tulizingatie.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi tukasema hapana, basi Mazrui tutakupa wewe ambapo kumbe umeme wako utakuwa ni ghali zaidi wakati kampuni ya Mhe. Moh'd Ali yake yeye inaweza ikafanya kazi ile ile na umeme huo ukawa nafuu zaidi. Kwa hivyo, jambo hili tunaliangalia vizuri ili atakayeweza kubahatika kuifanya hii kazi basi kile kitakachofanyika kiwe chenye manufaa kwa wananchi wetu ambapo haitakuwa mzigo.

Mhe. Moh'd Ali Salim amesema kwamba 'ndugu mkalie, usimtambie', kwa hoja ile ile ya kwamba 'nguo ya kuazima akasema haichezewi ngoma', yeye amekuwa mwalimu na sisi sote tunaelewa. Hofu hii kila mtu anayo na tuiangalie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nasema lazima tubadilike na Idara ya Nishati nayo ina kazi moja kubwa sasa hivi. Hivi karibuni Waheshimiwa Wajumbe timu yetu ilikwenda Arusha, tulipata nafasi ya kwenda kwenye maonesho kule. Tulikwenda kwenye banda moja kulikuwa kuna makaa yako pale yaliyokuwa yanatokana na hizi karatasi ambazo sisi sasa hivi tunazitia moto tukisha hapa. Mhe. Waziri hapa amechana zinatupwa, ni zile karatasi ambazo zimeshatumika, basi zinatengenezwa makaa na makaa hayo yanatumika. Hebu tuangalie ni tani ngapi za karatasi ambazo zimeshatumika tunazitupa na kuzitia moto tu ovyo, wakati upo uwezekano mkubwa wa kutumia karatasi ambazo hazifai tena zikatengenezwa makaa na zikapunguza uharibifu wa mazingira kwa kukata miti.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la matumizi ya umeme wa jua, tukiacha hii ya jumla, lakini kuna haja vile vile kwa baadhi ya wizara sasa hivi waelekee huko. Kwa mfano Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Mwembeladu na hisi *cottage hospital* zote, wana fursa kubwa ya kuwa na umeme wa *solar power*. Wenzetu sasa hivi kwa baadhi ya nchi wanaezeka nyumba zao kwa kutumia *solar panel* ambapo atakapokaa ameweza kuezeka nyumba yake hatovujiwa, lakini wakati huo huo anapata umeme kutoka kwenye lile paa la zile *solar panel*.

Mhe. Mwenyekiti, tuwashukuru wenzetu hawa wa Denmark kwa upande wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pale. Sasa hivi wale Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii paa lake kama wataliezeka kwa *solar panel*, basi hawatakuwa na hofu ya tatizo la umeme.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilikuwa naongea na wale madaktari wa Kichina walioondoka walikuwa wananiambia kuwa walikuwa na mpango wa hospitali ile ya Mkoani kuifanyia matengenezo na kuiezeka kwa *solar panel* ili kuondokana na tatizo hilo la kukosa umeme kila siku. Kwa hivyo, mambo haya yanawezekana kilichobaki ni kujituma.

Kama swahiba yangu pale nafikiri Sheikh Shaali alisema wakati mwengine sera hizi tunazitunga, tunazipitisha na zinaishia katika historia. Ni imani yangu kwa kupitia kwa Mhe. Waziri na watendaji hapa, sera hii ya nishati haitakuwa hivi, tutajitahidi kuifanyia kazi.

Jambo jengine ambalo sina hakika Mhe. Mazrui alilizungumza, sijui kama ni Mhe. Mazrui nimeshamsahau, juu ya matumizi haya ya hizi *bulb* tunazoziita *energy server*. Ni kweli kuna nchi zimepata mafanikio makubwa kwa kutumia *bulb* hizi na kuachana na *bulb* zetu za matungi. Lakini tatizo lililokuwepo, hebu Mhe. Mazrui tusaidie, nyinyi ni wafanyabiashara. Mhe. Mazrui unanisikia.

Mhe. Mwenyekiti, samahaniini. Wafanyabiashara serikali wakati mwengine inatoa unafuu wa kodi kwa baadhi ya vifaa, lakini nyinyi wafanyabiashara mnabaki pale pale, mnajua serikali ama imepunguza au kuondoa kodi kwa ajili ya *bulb* hizi, lakini mnachokifanya bei yenu imebaki pale pale. Shs. 1,500/-, Shs.2,500 na Shs.3,000/- kwa *bulb* moja.

Hiyo inawalazimisha kina Mhe. Tafana Kassim Mzee, Mhe. Mansour na wenziwe. Kwa mfano *bulb* yako imeungua saa 12 jioni au saa moja. Sasa unaamua utowe Shs. 1,500/- ukanunuwe *bulb* moja ile au utowe Shs. 250/- uwende ukanunuwe tungi lako la kawaida, nayo hii inachangia kwamba *bulb* hizi zimekuwa ghali mno, pamoja na kwamba imeondolewa kodi, lakini sisi wafanyabiashara bado hatukuchukua fursa hiyo tukapunguza bei ya bidhaa ile. Kwa hivyo, inalazimisha sasa watu wetu waendelee kutumia matungi haya ambayo ni rahisi, tofauti na ile Shs.1,500/- hadi Shs.3,000/-.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema kuna mambo haya tuyaangalie na tuyatizame. Sidhani kama itawezekana kupiga marufuku *bulb* hizi moja kwa moja na kuruhusu zile ziingie ikiwa bei yake iko hapo. Lakini nchi kama Cuba imefanikiwa sana, tena sana, sasa hivi takriban Wacuba wote wanatumia *bulb* hizi. Shirika la Umeme pale limeweka matangazo yake na watu wanayaelewa yote, sio kama hawaelewi, kwa kweli wanaelewa. Lakini aamuwe tu atowe Shs.3,000/- kwa tungi moja.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine namkata jina Mhe. Nassor Mazrui , huwa natumia jina la mkato hili ndio la umaarufu, nadhani halina neno Mhe. Mazrui.

Kwa hivyo, nataka nimalizie kwa kusema kwamba kila aliyepata fursa kuchangia sera hii ametoa mchango ambao ni madhubuti, unaoelezeka na unaotoa mwangaza wa nini la kufanya. Kwa hivyo, ni imani yangu michango yote ile ambayo Wajumbe wako wameitoa basi wizara hii kupitia kwa Mhe. Waziri ambaye baadae hapa atatoa maelezo yake pamoja na watendaji wengine wote, kweli tutaizingatia na kuona basi wale watakaokuja huko mbele wataifuata na kuitekeleza. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea kuwepo hapa tukiwa wazima wa afya na siha na kutujaalia kutupa uwezo sisi Wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar kuendelea na shughuli zetu kwa niaba ya wananchi wa visiwa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, Sera ya Nishati ya Zanzibar imechangiwa na Wajumbe 16, akianzia na:-

Mhe. Hamad Masoud Hamad
Mhe. Rashid Seif Suleiman
Mhe. Zakiya Omar Juma
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
Mhe. Abass Juma Muhunzi
Mhe. Haji Faki Shaali
Mhe. Ali Denge Makame
Mhe. Abubakar Khamis Bakary
Mhe. Juma Duni Haji
Mhe. Ali Abdalla Ali
Mhe. Abdalla Juma Abdalla
Mhe. Suleiman Hemed
Mhe. Ali Suleiman Ali
Mhe. Moh'd Ali Salim
Mhe. Said Ali Mbarouk
Mhe. Tafana Kassim Mzee

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wenzangu ninapokea pongezi na shukrani kwa kazi nzuri zinazofanywa na wizara yangu na mimi ninawarudishia pongezi hizo wenzangu ndani ya wizara wakitanguliwa na Mhe. Naibu Waziri. Kwa maana bila wao tusingeweza kufanikisha haya tuliyoweza kufanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza hili wamekiri kwamba sera imeandikika vizuri, imeyazingatia yote na mengi ambayo yanatarajiwa na wao na wananchi kupitia kwao. Hakuna maswali hasa yaliyoibuliwa, zaidi ni

msisitizo kwenye baadhi ya maeneo na kwa hivyo majumuisho yangu yatakuwa ni mafupi sana. Kwa hivyo, ninawaomba kwa heshima Wajumbe wanikubalie.

Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa nasaha zake na miongozo. Halikadhalika Mhe. Rashid Seif Suleiman Mhe. Zakiya Omar Juma na yeye kwa maelekezo yake na pongezi alizotoa kwa Ubalozi wa Norway na Serikali ya Rasilhema, tutawafikishia. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui naye namshukuru sana, alitaka tusome kutoka kwenye nchi za visiwa kama sisi ili tuelewe kwa nini umeme kwao una bei nafuu zaidi, ili na sisi tujifunze kutoka kwao kuhamisha uzoefu huo kwetu kwa ajili ya maslahi ya watu wetu tukiwa kwenye uchumi na kijamii.

Vile vile, alitoa indhari kama walivyotoa wengine wote juu ya mikataba hii ya mafuta na gesi. Suala hili tumelielezea kwa uwazi kabisa kwenye sera kwamba Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar ndio litakalothibitisha mikataba yote ya aina yote au mifumo yoyote ya nchi hii itaamua kwenda.Hayo ndio maamuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kupata nasaha na maoni yenu tangu huko tunakotoka na mijadala ya suala hili la mafuta na gesi asilia. Ndio iliyokuwa ahadi ya serikali kwamba suala hili litawekwa hadharani kutokana na yale tuliyoyazungumza udhoefu mbaya kwenye nchi nyengine za Afrika na kwengine duniani.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilifika pahala kusema kwa kipindi kile kwamba, pia tukizingatia historia yetu wenyewe ya kisiasa, mahusiano yetu ndani ya jamii ya Wazanzibari kuna umuhimu zaidi ya kuwa na uwazi huo. Bahati nzuri wakati tunamalizia hivi sasa Mhe. Said Ali Mbarouk amesema kwamba kufanikisha jambo hili linahitaji imani ya watu wote, linahitaji utulivu mkubwa wa kisiasa na inahitajika busara na hekima kubwa katika shughuli zetu za kijamii na kisiasa. Bila hivyo, hili kutekelezeka kwake ni ngumu sana, ni jambo sahihi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Haji Faki Shaali amezungumzia masuala ya *generator* ya akiba. Hilo nimelizungumza wakati nikijibu maswali leo asubuhi, alizungumza sawa sawa na ma-*generator* ya Pemba yale. Pia, alizungumzia Serikali ya Uganda kutoa *bulb* zile, nafikiri wewe ndiye uliyezungumza na ulitaka kujua ni kweli, kama nimekosea utanisaidia. Ni kweli nilipata taarifa kwamba kulikuwa kuna kipindi Serikali ya Uganda ilitoa karibu *bulb* 70,000 au 75,000 bure kwa wananchi, ili watumie *bulb* hizi zinazotumia umeme mdogo.

Vile vile, kama Wajumbe wengine, alitoa nasaha kwa Shirika la Umeme kuweza kutafakari kwa kina juu ya namna ya kupunguza bei kwa wananchi kuweza kuunga umeme. Suala hili tumelipokea kwa wote na tutalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Ali Denge Makame kama kawaida yake, kwa maelekezo na michango yake, huyu ni *professor* Ali Denge Makame na tutayafanyia kazi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary alitutanabahisha juu ya sheria nambari 3 ya mwaka 1998, masuala ya *equidistance principle*, masuala ya maji ya ndani na *territorial water* na kadhalika. Ninamshukuru sana Mhe. Abaubakar Khamis Bakary kwa sababu hii sio mara ya mwanzo, hata wakati tulipokuwa tunaanza mijadala hii alitutanabahisha na masuala haya. Naomba nikumbushe kwamba sote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tulikubaliana kwanza tuende na jambo moja la msingi, tufanye haraka kufanya maandiko kwa maana ya sera ambayo itaeleza 'kinaga ubaga' kwa lugha za siku hizi, au kama anavyozungumza Mhe. Ali Suleiman Ali 'kwa uwazi kabisa'. Nini msimamo wa Zanzibar juu ya masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, tukishakupata maandiko hayo na msingi huo, basi tuelekee kwenye masuala mengine.

Kwa hivyo, haya yote tunakushukuru sana kwa kutukumbusha tena, tunaelewa kwa sababu tumeshafanya huko nyuma. Pia, Mhe. Said Ali Mbarouk amezungumzia kwenye misingi hiyo hiyo *complex resolution*, kuwa na kampuni ya mafuta yetu wenyewe. Haya yote tunayategemea yatakuja kwenye sheria ya mafuta na pia kwenye hiyo mikataba ambayo nyinyi wenyewe mtakuja kuithibitisha PSA or *concision agreements* yoyote ile. Kwa hivyo, hilo litakuja na kama kawaida yetu tutashauriana kwa kila hatua na mtapata nafasi ya kutosha ya kuishauri serikali juu ya mwendo wa kwenda.

Mhe. Moh'd Ali Salim, pia alizungumzia nafikiri *by product* za mafuta kwamba tutazifanya nini? Hizo nazo zitaingia katika utaratibu huo huo.

Mhe. Juma Duni Haji alizungumzia juu ya taathira hii ya asilimia 82 ya nishati yetu kutokana na kuni na makaa. Mhe. Ali Abdalla Ali namshukuru na yeye alichukua hatua moja mbele akawajumuisha pia hawa wapasua mbao *furniture* hizi na mbao zinavyotumika kwa mambo mengine. Vile vile, akawa na wasi wasi kwamba hata hii asilimia 82 itazidi na tukitizama kinadharia ni sahihi kabisa. Kwa hivyo, bado kama inavyotuongoza sera umuhimu wa kuwa wabunifu na kuwa na mikakati. Suala hili napenda kuwahakikishia kwa sababu kuna mambo mlituagiza, tumeyafanyia kazi hata kabla sera haijaletwa kwenu.

Jambo la kwanza, ni kuanza kuwatafutia vijana wetu hii taaluma. Jambo hili tayari tumewaambia kuwa tumepata mfadhili na taasisi husika anafanyakazi. Pia, mlituelekeza juu ya kuelewa taathira ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta kwa wananchi wetu, wataathirika vipi na ardhi zao na wataathirika vipi na

shughuli zao za kijamii na shughuli zao za kiuchumi na hao watafidiwa na watafanywa nini na sekta nyengine zitaathirika vipi?

Jambo hili nalo tumeshalifanyia kazi. Pia, na masuala mengineyo ambayo mmetuelekeza. Kwa hivyo, hata kabla ya sera haijaletwa kwenu na kukubaliwa na nyinyi hii leo, tayari yale mliyotuelekeza tumeshaanza kuyafanyia kazi. Kwa hivyo, naomba niwahakikishie kwamba sera hii tutabuni mikakati ya kuiendeleza na pia atutakuwa wabunifu kuwa na ipitiwe mara kwa mara ili kuweza kukabiliana na hali tuliyokuwanayo.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi takriban wote mmezungumza kwamba ni lazima tufike pahala tuwe na kipaumbele, kwamba tufanye hili na mengine yasubiri na ndivyo itakavyokuwa katika mwelekeo wetu.

Mhe. Moh'd Ali Salim alizungumzia taathira ya hali tuliyokuwanayo kwa wanawake na watoto ni jambo la msingi sana. Yote uliyoeleza ni ya msingi, ni kweli, ni hali halisi ilivyo na ili kuokoa rasilimali hiyo ya watu, ni lazima kama nilivyoeleza tuwe na mikakati mbali ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, lakini pia tuwe wabunifu sasa kuwaondosha akinamama na watoto wa nchi hii katika hali hiyo ngumu na mbaya waliyonayo.

Pia, alizungumza suala la wafugaji kupata taaluma juu ya namna ya kutumia kinyesi cha mifugo yao, kwa ajili ya kuzalisha gesi pamoja na kupata mbolea. Kwa kweli ni jambo la msingi sana tena tunalikubali na tutalipa uzito wake kama ulivyotushauri *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, wengi miongoni mwa Waheshimiwa Wajumbe waliochangia walizungumza kuhusu suala la umuhimu wa hawa vijana tutakaowapeleka. Lakini waliokuwepo hivi sasa ambao wamekuwa watumishi waadilifu kwa serikali hii pamoja na Wazanzibari wenziwao, wamekubali kuwepo katika mazingira ambayo yapo kwa hivi sasa na huko nyuma.

Kwa hivyo, na wao wazingatiwe katika kupata kipaumbele kwenye masomo. Kwa kweli hilo tayari linafanyika na tutaendelea kuliwekea msisitizo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili. Kwa hiyo, tunakubali kwa heshima kubwa na unyenyekevu pongezi zao na mimi nakubali hizo kwa niaba ya wenzangu. Kutokana na hali hiyo tunaendelea kuwahakikishia kuwa tutajitahidi katika kuwa na mikakati mizuri zaidi ya kutekeleza wajibu wetu *(Makofi)*. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na Sera hii ya Nishati Zanzibar wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kama nilivyoonesha leo asubuhi kwamba nimefurahi. Kwa sababu mimi maisha huwa na furaha na wala sio mtu wa kununa, lakini leo nimefurahi zaidi *(Makofi)*.

Kwanza nataka nichukue fursa hii kwa sababu leo shughuli hizi za Baraza kesho zipo nyengine. Napenda kukupeni mkono wa mwaka mpya wa Kizungu na Kiislamu *(Makofi)*.

Vile vile, Waheshimiwa Wajumbe, napenda kukushukuruni kwa dhati kabisa kwa namna tulivyoingia Barazani safari hii, yaani tumeingia kwa mapenzi tunakumbatiana, tunacheka na kwenye michango ya leo pamoja na juzi tumeoonesha dhahiri kwamba ni watu wa moja. Kwa kweli hili ni jambo ambalo tulikuwa tukiliomba, miswada yote tumeipitisha *(Makofi)*.

Kwa hivyo, hii *spirit* ambayo tumeionesha basi tumuombe Mwenyezi Mungu atudumishe nayo, tupendane kwa sababu sisi sote ni Wazanzibari. Kwa kweli hakuna kitu kizito kama umoja. Kwa mfano tuliposhikana na kukubaliana wakati wa hoja ya mafuta, basi hoja ile tuliijadili hapa na kuikubali sote na ile ilitupa heshima *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wajumbe, wakati Mhe. Waziri Kiongozi alipokuwa akifunga Baraza aliahidi kuwa ameyasikia, atayachukua na kuyapeleka mbele. Mhe. Waziri Kiongozi hivi sasa hayo, lakini ametekeleza na amefanyakazi yake. Kwa hivyo, tumpe hongera.

Kwa sababu kazi yake ilizaa matunda wapi? Wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuwa akizungumza Pemba kwenye Sherehe za Mapinduzi alisema kwamba kuna hoja ambayo ilikuwepo Baraza la Wawakilishi na Wajumbe walichangia na serikali waliomba kuwa mafuta

yaondoshwe kwenye masuala ya muungano na yeye anaunga mkono na kushukuru *(Makofi)*.

Sasa na mimi namshukuru Mhe. Rais na alizungumza na Rais wa Jamhuri ya Muungano na wote walikubaliana. Kwa hivyo, hii ni ishara moja kwamba suala lile limepata nguvu kwa sababu ya umoja *(Makofi)*.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe niliona niseme hayo, ili tuondoke hapa kwa ajili ya kujenga nchi yetu. Kwa sababu hili ni Baraza la Wawakilishi na lazima lithaminiwe, lakini Baraza la Wawakilishi ndio ngome ya Wazanzibari, yaani ngome isiyotikisika. Kwa hivyo, kila mtu ajue akiwa ni Mjumbe, basi yeye ni sehemu moja ya nguzo ile *(Makofi)*.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe kuna matangazo, leo baada ya kuahirisha kikao cha Baraza kutakuwa na ziara ya kutembelea jengo jipya la Baraza la Wawakilishi huko Mbweni, ili Wajumbe wote waweze kuona maendeleo ya ujenzi huo.

Sasa mimi naongeza Wajumbe wote wa Baraza wakisimamiwa na Wanadhimu na kila mmoja ameleta barua ya dharura. Kwa hivyo, tunatakiwa baada ya Baraza kuahirisha kwenda Mbweni kwa ajili ya kuangalia ujenzi ule na hii ndio ziara yetu ya mwisho, kwa sababu watu wanataka kujua afisi zao na sehemu za kukaa. Kwa hiyo, mtu asijekusema aa! Mimi sina pa kukaa *(Kicheko/Makofi)*.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana sote na hii ndio ziara ya mwisho.Kwa hivyo, sote tushiriane na twende pale kwa ajili ya kupata muongozo wa mambo mbali mbali, ili ndani ya mwaka huu tukakae kule na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atajaalia tutakaa kule sote.

Waheshimiwa Wajumbe, kikao cha kesho kitakuwa na maswali na majibu. Vile vile, kutakuwa na Ripoti ya Uchunguzi wa Ajali ya Meli ya MV. Fatih na ripoti hiyo itagaiwa kwa Wajumbe leo hii. Vile vile, kesho kutwa siku ya Alhamis tarehe 28/01/2010 kutakuwa na maswali na majibu pia kutakuwa na Hoja Binafsi ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, naagiza nakla hizo zigaiwe leo *(Makofi)*.

Pamoja na hayo yote na mambo mazuri tuliyofanya leo, naomba hizi nyaraka zigaiwe, pia, tujiandae kwenda huko. Baada ya hayo, naliahirisha Baraza hili mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 5:40 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 27/01/2010 saa 3:00 asubuhi)